# HOTUBA YA WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI, MHESHIMIWA DKT. TITUS MLENGEYA KAMANI (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016

## 1.0 **UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, iliyochambua bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa kazi za Wizara kwa mwaka 2014/2015 na mwelekeo wa kazi za Wizara kwa mwaka 2015/2016. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

2. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Dkt Mohamed Gharib Bilal**, **Makamu** wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao imara wa kuanzisha na kusimamia mchakato wa kupata katiba

mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, napenda kuwapongeza Wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba kwa kufanikisha kukamilisha kupata katiba mpya. Tuna imani kuwa, wananchi watajitokeza kwa wingi kuipigia kura Katiba mpya ambayo itatufaa kwa kipindi cha miaka 50 ijayo. Aidha, nampongeza Mheshimiwa **Mizengo Kayanza Peter Pinda**, Mbunge wa Katavi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake imara na uliotukuka.

3. ***Mheshimiwa Spika***, naomba nichukue fursa hii kumshukuru kwa dhati, Mheshimiwa **Kaika Saning'o Ole Telele,** Mbunge wa Ngorongoro na Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa ushirikiano anaonipa katika kuendeleza Sekta za mifugo na uvuvi. Vilevile, napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Busega kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu. Pia, naishukuru familia yangu kwa kuendelea kunitia moyo ninapotekeleza majukumu ya kitaifa.

4. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya walioteuliwa na **Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kujiunga na Bunge lako tukufu ambao ni

**Mheshimiwa Dkt. Grace Khwaya Puja** na **Mheshimiwa Innocent Rwabushaija Sebba**.

5. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Mheshimiwa **Hayati Kapteni John Damian Komba** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbinga Magharibi. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya marehemu, ndugu na wananchi wa Jimbo alilokuwa analiwakilisha. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina. Aidha, naomba nitumie fursa hii kuwakumbuka wananchi wenzetu waliopoteza maisha kutokana na mafuriko, ajali na sababu mbalimbali.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua fursa hii kumshukuru **Mhe. Profesa Peter Mahamudu Msolla,** Mbunge wa Kilolo na **Mhe. Said Juma Nkumba**, Mbunge wa Sikonge pamoja na wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushauri, maoni, maelekezo na ushirikiano waliotupatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na maandalizi ya bajeti hii. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu itaendelea kuzingatia ushauri, mapendekezo na maoni ya Kamati na yale yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, **Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda**, Mbunge wa Katavi kwa hotuba yake nzuri yenye kutoa malengo ya Serikali na mwelekeo wa utendaji wa sekta mbalimbali pamoja na kazi za Serikali kwa mwaka 2015/2016. Aidha, nachukua nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote waliotoa hotuba zao ambazo zimeainisha maeneo mbalimbali tunayoshirikiana katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi nchini. Vilevile, nawashukuru waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao kuhusu masuala ya maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi kupitia hotuba hizo.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM 2010

8. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza majukumu ya sekta za mifugo na uvuvi, Wizara imezingatia maelekezo yaliyomo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010. Ilani inatambua mchango mkubwa unaoweza kutolewa na sekta hizi katika kuwapunguzia wananchi umaskini na kuongeza Pato la Taifa.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** ili Sekta ya Mifugo iweze kutoa mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa, Serikali imeelekezwa kutekeleza yafuatayo:-

**Mapinduzi ya Ufugaji**

(i) *Serikali iandae programu kabambe ya kuendeleza sekta ya mifugo na ufugaji. Programu hiyo ijumuishe pamoja na mambo mengine masuala ya uendelezaji WA maeneo ya malisho, kuchimba na kujenga malambo, mabwawa, majosho na huduma za ugani ili hatimaye wafugaji waondokane na ufugaji wa kuhamahama.*

**Utekelezaji:**

Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa na kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo (2010) na Programu ya Kuendeleza Sekta za Mifugo ya mwaka 2011 ambayo imejumuisha masuala ya uendelezaji wa maeneo ya malisho, malambo, mabwawa, majosho na huduma za ugani. Programu hii imejumuishwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka mitano (2011/2012-2015/2016). Programu hii inatekelezwa kupitia bajeti ya Wizara na taasisi kila mwaka.

(ii) *Benki ya Kilimo itakayoanzishwa iwe pia Benki ya Mifugo ili iweze kutoa mikopo kwa wasomi wenye nia ya kufuga na kuwawezesha kuingia kwa wingi katika ufugaji wa kisasa.*

**Utekelezaji:**

Wizara inaendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha, Kilimo Chakula na Ushirika kuanzisha Benki ya Kilimo itakayotoa mikopo kwa wadau wa sekta ya mifugo. Benki hii itaanza kazi rasmi Mwezi Julai, 2015. Kwa sasa, Wizara inaendelea kuhamasisha wafugaji wakiwemo wasomi kutumia uwepo wa dirisha dogo katika Benki ya Taifa ya Rasilimali kukopa fedha kwa ajili ya kuendeleza ufugaji wa kisasa.

(iii) *Kuelimisha wafugaji kuhusu umuhimu wa uwiano kati ya idadi ya mifugo na eneo.*

**Utekelezaji:**

Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imeendelea kuelimisha wafugaji kuhusu kutekeleza Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo Na. 13 ya mwaka 2010 ambayo, pamoja na mambo mengine, inawataka wafugaji kufuga mifugo kulingana na uwezo wa ardhi; kutunza malambo na vyanzo vya maji; kuendeleza na kuhifadhi malisho; na kutenga maeneo ya akiba kwa ajili ya kiangazi.

Aidha, Wizara inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu uwiano wa matumizi ya rasilimali za malisho na maji kulingana na ongezeko la idadi ya watu na mifugo kwa kuainisha maeneo ya malisho na kufanya tathmini ya uwezo wake, kutangazwa kwenye gazeti la Serikali na kulindwa kwa mujibu wa sheria kwa kushirikisha wadau. Hadi sasa, maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya ufugaji ni hekta **milioni 1.95** katika Mikoa **22,** Wilaya **81** na vijiji **620** mwaka 2015**.** Pia, Wizara imeendelea kuhamasisha wafugaji na sekta binafsi kuzalisha malisho bora ya mifugo ambapo idadi ya wazalishaji binafsi wa malisho bora wameongezeka kutoka wawekezaji sita (**6)** mwaka 2009/2010 hadi **40** mwaka 2014/2015 na kuwezesha uzalishaji wa marobota kutoka **69,100** mwaka 2009/2010 hadi **1,098,311** ya hei mwaka 2014/2015.

(iv) *Serikali isimamie kwa ufanisi mkubwa mradi wa kopa ng'ombe/mbuzi, lipa ng'ombe/mbuzi kama hatua ya kueneza ufugaji wa kisasa wenye tija kubwa.*

**Utekelezaji:**

Wizara imewezesha upatikanaji wa mitamba bora ya maziwa **70,862** kupitia Mashamba ya Kuzalisha Mitamba ya Kitulo, Mabuki, Nangaramo, Ngerengere na Sao Hill pamoja na

Ranchi za NARCO na Mipango ya Kopa Ng'ombe lipa Ng'ombe. Vilevile, mbuzi wa maziwa **12,017** wamesambazwa kupitia Mpango wa Kopa Mbuzi lipa Mbuzi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Bill and Melinda Gates Foundation imeanzishwa mradi Kuendeleza tasnia ya Maziwa kwa nchi za Afrika ya Mashariki (The East Africa Dairy Development – EADDII) unaotekelezwa katika Mikoa ya Njombe (Njombe Mjini, Njombe Vijijini na Wanging'ombe), Mbeya (Rungwe, Mbozi, Mbeya na Busokelo) na Iringa (Iringa Vijijini, Kilolo na Mufindi) ambao utasaidia kuongeza idadi ya ng'ombe wa maziwa kupitia mradi wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe.

*(v) Kuendeleza elimu kwa wafugaji ili wajue kuwa mifugo waliyonayo ni mali inayoweza kuvunwa katika umri na uzito muafaka unaokidhi mahitaji ya soko, ili kuwaondolea umaskini wao badala ya kuridhika na wingi wa mifugo iliyo duni na maisha ya kuhamahama.*

**Utekelezaji:**

Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na Asasi mbalimbali kama vile *Land O' Lakes, Heifer Project Tanzania (HPT), World Vision na Care Tanzania* imetoa mafunzo kwa wafugaji **35,796** kuhusu mbinu za ufugaji bora wa mifugo. Aidha, jitihada za makusudi za

kuchochea uvunaji na uuzaji wa mifugo na mazao yake katika maeneo ya wafugaji zimefanyika kwa kuwekeza katika ujenzi wa machinjio ya kisasa Simanjiro, Monduli, Dodoma, Magu, Bagamoyo, Ruvu, Mwanza, Kagera, Shinyanga, Morogoro na Iringa. Pia, viwanda vya kusindika maziwa vimejengwa Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Njombe, Mwanza, Iringa, Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Kagera na kwa lengo hilo hilo. Aidha, miongozo ya unenepeshaji imeandaliwa na kusambazwa kwa wafugaji ambapo unenepeshaji wa ng'ombe umeongezeka kutoka ng'ombe **62,000** mwaka 2010 hadi **175,000** mwaka 2014. Unenepeshaji huo unafanyika katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Geita, Arusha, Rukwa, Tabora, Tanga, Pwani na Kilimanjaro.

*(vi) Uzalishaji wa mitamba upanuliwe kwa kiwango kikubwa kwa Serikali kuvutia na kuwezesha sekta binafsi katika uzalishaji na ufugaji wa kisasa.*

**Utekelezaji:**

Wizara imeendelea kuboresha mashamba ya kuzalisha mitamba ya Mabuki, Nangaramo, Ngerengere na Sao Hill na Kitulo ili yaweze kuzalisha mitamba **5,000** kwa mwaka. Aidha, Serikali imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa mitamba kwa kuwapatia mafunzo ya mbinu za ufugaji bora na

ziara za mafunzo ndani na nje ya nchi. Kwa sasa, sekta binafsi imezalisha na kusambaza zaidi ya mitamba **15,000**.

*(vii) Kufufua na kujenga majosho na malambo mapya kwa ajili ya mifugo na kuhimiza uogeshaji endelevu.*

**Utekelezaji:**

Jumla ya majosho **136** yalijengwa kwa gharama ya **shilingi 2,965,687,765**/= Aidha, majosho **111** yalikarabatiwa kwa jumla ya **shilingi 977,520,950/=.** Pia, ili kuhimiza uogeshaji endelevu, Serikali ilinunua lita **252,138** za dawa za kuogesha mifugo kwa kutoa ruzuku ya shilingi **bilioni 4.2** na kuzisambaza katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa nchini. Wafugaji wananunua dawa hizo kwa asilimia **60** ya bei ya soko na asilimia **40** iliyobaki inalipwa na Serikali kama ruzuku.

*(viii) Kuimarisha utafiti wa mifugo kwa kuboresha na kuhifadhi kosaafu za mifugo ya asili ili kuongeza uzalishaji endelevu.*

**Utekelezaji:**

Wizara imeimarisha utafiti wa mifugo wenye lengo la kuboresha na kuhifadhi kosaafu za mifugo ya asili kwa kukusanya na kuchambua takwimu mbalimbali za maendeleo ya ukuaji na

uzalishaji kwa mbari za mifugo ya asili kwa mifugo ifuatayo:

(a) Ng'ombe **44** wa aina ya *Ufipa*, **3O** aina ya *Ankole*, na **20** aina ya *Singida White* wamehifadhiwa na utafiti unaendelea, ambapo matokeo ya awali yameonesha kwamba ng'ombe aina ya ufipa anafikia wastani wa kilo **400** kwa madume na **280** kwa majike katika umri wa miaka 4;

(b) Mbuzi **60** aina ya *Pare White,* **30** *Sonjo Red,* **93** *Gogo White,* **125** *Newala* na Kondoo **100** aina ya *Red Maasai* wamehifadhiwa na utafiti unaendelea, ambapo matokeo yameonesha kwamba *Gogo white* wanafikia wastani wa kilo **50** kwa madume na majike kilo **40** katika umri wa miaka 3; na

(c) Kosaafu za mbari za kuku **50** wa *Kawaida,* **35** *Sasamala,* **45** *Kishingo,* **41** *Kisunzu,* **39** Bukini, **39** *Kuchi,* **25** *Mtewa,* **26** *Kuza,* **49** *Sukuma,* **41** *Msumbiji* na **26** *Njachama* wamehifadhiwa na utafiti unaendelea, ambapo matokeo yameonesha kwamba *kuchi* anafikia wastani wa kilo **2.7** kwa jogoo na makoo kilo **1.7** kwa umri wa

miezi 18. Aidha, *kishingo* ameonesha kutoa mayai **18** kwa mtago mmoja.

*(ix) Kuimarisha huduma za ugani na mafunzo ya watalaam na wafugaji.*

**Utekelezaji:**

Wizara imeendelea kuimarisha huduma za ugani na mafunzo ya watalaam na wafugaji kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuimarisha Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA) kwa kuboresha miundombinu na kuongeza idadi ya vyuo vya mafunzo kutoka sita (6) hadi nane (8) na hivyo kuongeza udahili kutoka **1,498** mwaka 2010/2011 hadi **2,451** mwaka 2014/2015;

(b) Jumla ya wafugaji **9,016** wamepata elimu juu ya ufugaji wa kisasa na endelevu;

(c) Maafisa ugani wa mifugo wameongezeka kutoka **2,587** mwaka 2010/2011 hadi **8,541** mwaka 2014/2015; na

(d) Kuimarisha rasilimali watu kwa kuwezesha wakufunzi **42** kuhudhuria mafunzo katika ngazi ya shahada ya Uzamivu watatu (**3**), shahada ya uzamili

(**16)**, shahada ya kwanza (**19)**, stashahada (**4**).

(x) *Kuongeza na kuimarisha vituo vya uzalishaji mbegu bora za mifugo na kuhimiza matumizi ya mbegu hizo.*

**Utekelezaji:**

Wizara imeendelea kuimarisha vituo vya uzalishaji mbegu bora za mifugo na huduma za uhimilishaji kwa kuimarisha  Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji – NAIC Usa River na vituo sita (**6**) vya Kanda vya Mbeya, Katavi, Mwanza, Kibaha, Dodoma, na Lindi. Aidha, kituo cha pili cha Taifa cha Sao Hill kinaendelea kujengwa. Vilevile, madume bora ya mbegu **24** aina ya Ayrshire (**11**), Friesian (**8**), Jersey (**3**), Sahiwal (**1**) na Simmental (**1**) kutoka Kenya na madume aina ya Mpwapwa manne (**4**) na Boran (**4**), yamenunuliwa kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mbegu bora katika kituo cha NAIC Arusha; na dozi **685,290** za mbegu bora zimezalishwa na kusambazwa kwa wafugaji na wataalam **1,246** kutoka maeneo mbalimbali nchini wamepata mafunzo ya uhimilishaji. Kutokana na juhudi hizi, uhimilishaji umeongezeka kutoka ng'ombe **73,900** mwaka 2010/2011 hadi **175,000** mwaka 2014/2015.

(xi) *Kuimarisha huduma za afya ya mifugo kwa kudhibiti magonjwa ya mifugo hasa ya milipuko na uanzishwaji wa Maeneo Huru kwa Magonjwa ya Mifugo.*

**Utekelezaji:**

Wizara imeendelea kuimarisha huduma za afya ya mifugo na udhibiti wa magonjwa ya milipuko kwa:-

(a) Kuchanja ng'ombe **milioni 7.2** dhidi ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe *(CBPP*);

(b) Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti Ugonjwa wa Miguu na Midomo ambapo hatua ya awali ilikuwa ni utambuzi wa aina ya vimelea vinavyosababisha ugonjwa huo. Jumla ya sampuli **2,740** za ng'ombe na **322** za wanyama pori zilichukuliwa;

(c) Kushirikiana na Halmashauri za Mikoa ya Mbeya, Iringa na Dar es Salaam katika kudhibiti Homa ya Nguruwe ambapo dawa za kupulizia lita **400** zilinunuliwa na kupelekwa kwenye Halmashauri zilizoathirika. Ugonjwa huu umedhibitiwa kwenye maeneo hayo, hata hivyo ugonjwa huo umeonekana kwenye

maeneo mapya ambayo ni Itigi (Manyoni) na Katubuka (Kigoma); na

(d) Mkakati wa Kudhibiti Mafua Makali ya Ndege umeendelea kutekelezwa ambapo Mpango wa Tahadhari na Udhibiti umeandaliwa. Hata hivyo, ugonjwa haujaingia nchini.

*(xii) Kuhimiza wafugaji kutekeleza kanuni za ufugaji bora na kuingia katika ufugaji endelevu wa kisasa na kibiashara unaozingatia hifadhi ya mazingira.*

**Utekelezaji:**

Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na wadau wengine imeendelea kuhamasisha wafugaji kufuga kisasa kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa elimu kwa wafugaji **90,160** kuhusu kanuni za ufugaji bora, uzalishaji ng'ombe bora wa nyama na maziwa, unenepeshaji, ufugaji bora wa mbuzi, kondoo, nguruwe na wanyama wengine pamoja na uzalishaji na uhifadhi wa malisho bora;

(b) Kuhamasisha sekta binafsi kuzalisha malisho bora ambapo marobota **2,373,302** ya hei yamezalishwa; na

(c) Kushirikiana na wadau wengine wakiwemo taasisi za BRAC, US-GRAIN na Maadili Centre kuhamasisha na kuwezesha ufugaji bora wa kuku wa asili na jamii nyingine za ndege kwa kuwapatia huduma za ugani ikiwa ni pamoja na kusambaza chanjo ya mdondo, kuwapatia wafugaji vifaranga vya kuku wa asili kupitia mikataba ya kibiashara, kutoa elimu ya ufugaji wa kibiashara na kuwaunganisha na soko.

*(xiii) Kuhamasisha uanzishaji na uimarishaji wa vikundi vya ushirika wa wafugaji.*

**Utekelezaji:**

Wizara imeendelea kuhamasisha uimarishaji wa vikundi vya wafugaji ambapo jumla ya vikundi **154** vya wafugaji vimeundwa. Lengo ni kuwa na vikundi ambavyo vinaweza kusajiliwa na hivyo kuwa na uwezo wa kupata mikopo, kuwa na nguvu kwenye soko kuhusu bei ya mazao yao na kupata elimu ya ufugaji bora na wa kibiashara kwa pamoja.

*(xiv) Kuhamasisha ushirikishwaji wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma mbalimbali za mifugo.*

**Utekelezaji:**
Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania imeendelea kuhamasisha, kuratibu na kusajili na kusimamia watoa huduma wa afya ya mifugo kutoa huduma hizo. Katika kipindi cha mwaka 2009/10 hadi 2014/15 jumla ya vituo **315** vya huduma ya afya ya mifugo vya sekta binafsi vimesajiliwa. Vituo hivi vimetoa ajira kwa watoa huduma **1,775** na vimeendelea kutoa huduma ya afya ya mifugo ikiwemo ushauri, tiba na chanjo kwa mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa sekta ya uvuvi, Ilani imeelekeza sekta hii kuwa ya kisasa zaidi na iweze kuchangia mchango mkubwa kwenye pato la Taifa. Hivyo, Serikali imeelekezwa kutekeleza yafuatayo:-

**Mapinduzi ya Uvuvi**

*(i) Wizara ianzishe na kuendesha vyuo vyake vya uvuvi ili iweze kuandaa wataalamu wengi wa Sekta ya Uvuvi*

**Utekelezaji:**

Wizara imeimarisha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) kwa kuboresha miundombinu na kuongeza idadi ya vyuo vya mafunzo kutoka vyuo viwili (**2**) vya FETA Nyegezi na FETA Mbegani hadi vyuo vitano (**5**) vya FETA

Nyegezi (Mwanza), Mbegani (Pwani), Gabimori (Mara), Kibirizi (Kigoma) na Mikindani (Mtwara). Aidha, kituo cha Mwanza South kimefanywa kituo cha kuendesha masomo chini ya FETA Nyegezi. Kutokana na hatua hizi udahili umeongezeka kutoka wanachuo **425** mwaka 2011/2012 hadi wanachuo **1,180** mwaka 2014/2015.

*(ii) Kuweka ulinzi madhubuti wa bahari zetu dhidi ya wavuvi haramu ikiwa ni pamoja na kukamata vyombo vyao vya uvuvi na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria.*

**Utekelezaji:**

Wizara imefanya mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni za Uvuvi na miongozo mbalimbali ambapo rasimu ya Sera mpya imekwisha andaliwa na kupitishwa na Baraza la Mawaziri Februari 2015; Vile vile mapitio ya Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 yamefanyika ili kuongeza ufanisi wa usimamizi wa rasilimali za uvuvi na kukidhi mahitaji halisi ya sasa; Kuanzisha mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya mwaka 1994 ambapo rasimu ya marekebisho ya Sheria hii imewasilishwa katika Kamati ya Makatibu Wakuu; na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Na. 6 ya Mwaka 1980 imekwisha kuridhiwa na Baraza la Mawaziri.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi katika bahari ya ndani na maeneo mengine ya uvuvi. Vilevile, Wizara imewezesha ununuzi wa boti **24** za doria na kuzisambaza katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo; Halmashauri za Bagamoyo (**1**), Lindi Vijijini (**1**), Pangani (**1**), Mkinga (**1**), na Mkuranga (**1**); Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (Mnazi Bay Mtwara (**1**), Mafia (**1**), Dar es Salaam (**2**) na Silikanti-Tanga (**1**)); Wizara ya Maliasili na Utalii - Idara ya Misitu na Nyuki (**2**), vituo vya doria vya Dar es Salaam (**1**), Mafia (**1**), Tanga (**1**), Mtwara (**1**), Kigoma (**2**), Kasanga (**2**), Ikola (**1**), Kipili (**1**), Buhingu (**1**) na Mbamba bay (**1**). Pia, vifaa vingine vilinunuliwa vikiwemo pikipiki (**6**), baiskeli (**10**) na jenereta (**2**) kwa ajili ya vituo vya doria vya Kasanga **(1)** na Mbamba bay **(1)**.

(iii) *Kuandaa na kutekeleza programu yenye malengo yanayopimika mwaka hadi mwaka kuhusu haja ya kuleta mapinduzi ya uvuvi yanayotumia zana na maarifa ya kisasa.*

**Utekelezaji:**

Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Uvuvi imeandaa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Uvuvi ambayo inatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2011/2012 hadi 2015/2016 kupitia bajeti ya kila mwaka ya

Wizara. Pia, mipango na mikakati mbalimbali ya usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi iliandaliwa na kutekelezwa ikiwemo Mpango wa usimamizi wa samaki wanaopatikana katika tabaka la juu la maji (Artisanal Pelagic Fisheries Management Plan) na Mkakati wa usimamizi wa samaki aina ya Jodari (Tanzania Tuna Fishery Management Strategy).

*(iv) Kuimarisha ushirikishwaji wa jamii na wadau katika ulinzi, usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi.*

**Utekelezaji:**
Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa imeendelea kuwashirikisha wadau katika ulinzi na usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi kwa kuanzisha Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (Beach Management Unit-BMUs) **749** katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, miongozo ya kuanzisha Maeneo ya Usimamizi wa Pamoja (Guidelines for Establishment Collaborative Fisheries Management Areas) imeandaliwa na maeneo matatu (**3**) katika Wilaya za Mafia, Rufiji na Kilwa yameanzishwa. Pia, BMUs zimeendelea kuimarishwa kwa kupewa elimu na mafunzo mbalimbali kuhusu uvuvi endelevu, ukusanyaji wa takwimu za uvuvi, uhifadhi wa mazao ya uvuvi na mazingira kwa ujumla.

(v) *Kuimarisha miundombinu ya uvuvi kwa kujenga mialo, masoko ya kisasa, vituo vya kutotolea vifaranga vya samaki na maabara.*

**Utekelezaji:**

Wizara imeendelea kuimarisha miundombinu ya uvuvi kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Wizara imejenga na kuboresha mialo mitatu (**3**) ya kisasa ya kupokelea mazao ya uvuvi katika Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi chini ya mradi wa Usimamizi wa Rasilimali za Bahari na Ukanda wa Pwani (Marine and Coastal Environmental Management Project – MACEMP). Mialo hiyo ni Kilindoni (Mafia), Nyamisati (Rufiji) na Masoko Pwani (Kilwa);

(b) Katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika kupitia Programu ya Usimamizi wa Bonde la Ziwa Tanganyika (PRODAP) uliokuwa unaratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) uliotekelezwa kuanzia mwaka 2008 hadi Desemba 2013, mialo minne (**4**) ya kupokelea samaki ya Kibirizi (Ujiji-Kigoma), Muyobozi (Kigoma Vijijini), Ikola (Mpanda Vijijini) na Kirando (Nkasi)

imejengwa na imekabidhiwa kwa Halmashauri husika;

(c) Katika Ukanda wa Ziwa Victoria mialo **19** ilikarabatiwa na mialo **6** ya kisasa ilijengwa chini ya Mradi wa Implementation of Fisheries Management Plan (IFMP) katika maeneo ya Marehe (Missenyi), Kikumbaitare (Chato), Bwai (Musoma), Sota (Rorya), Kigangama (Magu) na Kahunda (Sengerema);

(d) Wizara kupitia Halmashauri ya Sumbawanga kwa kushirikiana na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) imejenga Soko la Samaki Kasanga ambalo litawezesha wavuvi kupata soko la uhakika la kuuzia mazao yao na kuongeza kipato; na

(e) Mafunzo kuhusu taratibu na kanuni za usafirishaji wa samaki hai nje ya nchi kwa wasafirishaji wadogo **40** kusisitiza umuhimu wa kuwa na vibali pamoja na leseni halali ili kuongeza pato la taifa na kutokomeza biashara haramu ya mazao ya uvuvi na kwa wafanyabiashara **18** wanaoingiza mazao ya uvuvi nchini kuhusu uhifadhi na utunzaji wa samaki ili kulinda afya ya mlaji na soko.

(vi) *Kuboresha mazao ya uvuvi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.*

**Utekelezaji:**
Wizara imeendelea kusimamia ubora na viwango kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi kama ifuatavyo:-

(a) Kufanya kaguzi na kutoa mafunzo ambapo jumla ya kaguzi **2,800** zilifanyika kuhakiki mazao ya uvuvi yanayosafirshwa nje ya nchi;

(b) Kufanya kaguzi **519** kwenye viwanda vinavyosindika minofu ya samaki na maghala ya kuhifadhi mazao ya uvuvi ili kuhakiki viwango vya uzalishaji na uhifadhi wa mazao ya uvuvi;

(c) Kufanya chunguzi za kimaabara kwa sampuli **694** za samaki, maji, vyakula vya samaki na udongo ili kubaini uwepo wa vimelea vinavyosababisha magonjwa, mabaki ya viuatilifu, madini tembo na *antibiotics* kabla ya kumfika mlaji; na

(d) Kuimarishha Maabara ya Samaki Nyegezi kwa kuipatia vitendea kazi na kukamilisha maandalizi ya Miongozo ya Utendaji (*Standard Operating Procedures – SOP).*

(vii) *Kujenga mazingira ya kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi hususan ujenzi wa viwanda vya samaki.*

**Utekelezaji:**

Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya uvuvi ikiwa ni pamoja na kujenga viwanda vya kuchakata samaki ambapo hadi kufikia mwaka 2014/2015 viwanda **48** na maghala **84** ya kuhifadhi mazao ya uvuvi yamejengwa. Aidha, Wizara imeimarisha Maabara ya Taifa ya Kudhibiti Ubora wa Mazao ya Uvuvi Nyegezi kwa kuipatia vitendea kazi na kuwajengea watumishi uwezo. Pia, Wizara imetoa mafunzo kuhusu teknolojia mbalimbali za uhifadhi na uchakataji wa mazao ya uvuvi kwa wadau **1,493** kutoka Halmashauri za Jiji la Mwanza (**185**) na Tanga (**90**), Manispaa za Bukoba **(180)**, Musoma **(150)**, Ilala (**44**), Kigoma – Ujiji (**24**) na Sumbawanga (**50**); na Halmashauri za Pangani (**40**), Muheza (**120**), Mafia (**80**), Mtwara Vijijini (**52**), Lindi Vijijini (**78**), Mkuranga (**50**), Bagamoyo (**40**), Nkasi (**130**) na Mpanda (**80**).

(viii) *Kuhamasisha wawekezaji wa ndani na wa nje kuwekeza katika uvuvi kwenye Bahari Kuu.*

**Utekelezaji:**

Serikali imeendelea kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika uvuvi Bahari Kuu. Katika kufikia lengo hili Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bandari pamoja na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu imeandaa Hadidu za Rejea za kufanya upembuzi yakinifu wa kujenga bandari ya uvuvi na kusambaza kwa washauri elekezi watakaofanya kazi hiyo. Bandari inatarajiwa kujengwa mwambao wa pwani na itawezesha kuongeza mapato, ajira na upatikanaji wa samaki. Aidha, Wizara kupitia FETA na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu ilitoa mafunzo kwa wavuvi **100** kuhusu uvuvi katika Bahari Kuu.

*(ix) Kuimarisha na kuendeleza uanzishwaji wa maeneo tengefu kwenye maziwa makuu hususani Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa*

**Utekelezaji:**

Serikali imeandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya mwaka 1994 ili kuanzisha Hifadhi na Maeneo Tengefu katika maji baridi.

(x) *Kuhamasisha uimarishaji na uanzishaji wa vikundi vya ushirika wa wavuvi na wafugaji wa samaki*

**Utekelezaji:**

Wizara imeendelea kuhamasisha jamii za wavuvi kupitia mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na miradi mbalimbali kujiunga kwenye vikundi vya akiba na mikopo ambapo jumla ya vikundi **208** vimeanzishwa katika Halmashauri za Temeke (**32**), Rufiji (**34**), Mafia (**61**), Mtwara (**21**) na Kilwa (**60**) vyenye jumla ya wanavikundi **5,573**. Aidha, vipindi **52** vya redio na **20** vya luninga vya uhamasishaji na uanzishaji wa vikundi vimeandaliwa na kurushwa, vitabu **2,000** na vipeperushi **4,000** vimeandaliwa na kusambazwa. Pia, elimu ya ufugaji samaki uwiano na kilimo imetolewa kwa wadau **1100** ikizingatia udhibiti wa matumizi ya maji yaliyopo kwenye mabwawa na mabaki ya mimea ya shambani ili kuzuia uchafuzi wa mazingira. Vilevile, ufuatiliaji na ukaguzi wa shamba la Kambamiti la Alphakhrust-Mafia lenye mabwawa **30** umefanyika ili kuzuia na kudhibiti magonjwa ya Kambamiti pamoja na kuzingatia uhifadhi wa mikoko kwenye eneo la shamba hilo.

*(xi) Kuimarisha usimamizi wa mazingira katika maeneo ya Uvuvi, ukuzaji viumbe kwenye maji na maeneo tengefu.*

**Utekelezaji:**

Wizara kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) imeendelea kuimarisha usimamizi wa mazingira na rasilimali za uvuvi kwa kutoa elimu kwa wananchi waishio ndani na kandokando ya Hifadhi za Bahari tatu **(3)** na maeneo Tengefu **15**. Vile vile, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 - 2014/2015 MPRU imetangaza visiwa vinne **(4)** vya Kirui, Kwale, Mwewe na Ulenge vilivyoko mkoani Tanga kuwa Maeneo Tengefu. Aidha, katika kuimarisha utalii MPRU imeingia mikataba minne **(4)** na wawekezaji wa ndani na nje kujenga eco-lodge katika visiwa vya Kirui/Mwewe-Tanga, Mbudya-Dar es Salaam na Shungumbili-Mafia.

*(xii) Kuhimiza shughuli mbadala za kiuchumi kwa jamii za wavuvi ili kupunguza shinikizo la uvuvi kwenye maji ya asili na maeneo tengefu*

**Utekelezaji:**

Wizara imeendelea kuhamasisha wananchi kuendesha shughuli mbadala za kiuchumi ambapo kwa upande wa Ukanda wa Pwani

jumla ya vikundi **230** viliwezeshwa kupitia mradi wa MACEMP kutekeleza miradi mbadala ya kiuchumi ikiwemo ufugaji nyuki, ufugaji samaki, kilimo cha bustani, ufugaji ng'ombe, mbuzi na kuku, ukulima wa mwani, ususi, ushonaji pamoja na usindikaji wa chumvi.

## 3.0 HALI YA SEKTA ZA MIFUGO NA UVUVI NA CHANGAMOTO ZILIZOPO

### Sekta ya Mifugo

10. ***Mheshimiwa Spika***, sekta ya mifugo ni muhimu katika kumwondolea mwananchi umaskini. Mifugo hutoa ajira, lishe, nishati, mbolea na hutumika kama wanyamakazi na benki hai. Kulingana na takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu mwaka 2014, sekta ya mifugo ilikua kwa asilimia **2.2** ikilinganishwa na asilimia **2.0** mwaka 2013. Aidha, kulingana na takwimu zilizopo, idadi ya mifugo nchini inakadiriwa kuwa ng'ombe **milioni 25.8**, mbuzi **milioni 16.7** na kondoo **milioni 8.7.** Pia, wapo kuku wa asili **milioni 37.0,** kuku wa kisasa **milioni 32.0** na nguruwe **milioni 2.4.**

Aidha, ulaji wa mazao ya mifugo kulingana na viwango vya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO, 2011) ni kilo **50** za nyama, lita **200** za maziwa na mayai **300** kwa mtu kwa mwaka. Kwa upande wa nchi yetu viwango vya ulaji wa mazao hayo kwa sasa ni

wastani wa kilo **15** za nyama, lita **47** za maziwa na mayai **106** kwa mtu kwa mwaka.

**Sekta ya Uvuvi**

11. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli za uvuvi hufanyika katika maeneo yote ya maji baridi na maji chumvi. Eneo la maji baridi linajumuisha maziwa makuu ambayo ni; Ziwa Victoria (kilometa za mraba **35,088**), Ziwa Tanganyika (kilometa za mraba **13,489**) na Ziwa Nyasa (kilometa za mraba **5,700**), mabwawa, maziwa ya kati na madogo **45**, mito **29** na maeneo oevu. Pia, nchi yetu ina ukanda wa pwani wa Bahari ya Hindi wenye urefu wa kilometa **1,424** ambao umegawanyika katika eneo la Maji ya Kitaifa (Territorial Sea) lenye ukubwa wa kilometa za mraba **64,000** na eneo la Bahari Kuu lenye ukubwa wa kilometa za mraba **223,000**.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya uvuvi huchangia katika upatikanaji wa lishe bora, ajira, kipato kwa wananchi na pato la Taifa na hivyo kuchangia katika kuondoa umaskini. Sekta hii imepungua kwa asilimia **2.0** mwaka 2014 kutoka asilimia **5.5** mwaka 2013. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kumechangiwa na kupungua kwa soko la samaki na samaki nje ya nchi na matumizi ya nyenzo duni za uvuvi Aidha, mchango wa Sekta hii kwa pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia **1.4** mwaka 2013

mpaka asilimia **2.4** kwa mwaka 2014. Vilevile, katika mwaka 2014/2015, idadi ya wavuvi wadogo imeongezeka kufikia **183,800** ikilinganishwa na wavuvi **183,341** mwaka 2013/2014. Kutokana na kuongezeka kwa shughuli za uvuvi ikiwa ni pamoja na ongezeko la wananchi wanaotegemea shughuli za uvuvi katika kujipatia kipato zikiwemo biashara ya samaki, uchakataji wa mazao ya uvuvi, utengenezaji wa zana na vyombo vya uvuvi na biashara nyingine zinazohusiana na sekta ya uvuvi.

**Changamoto**

13. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kasi ndogo katika kumilikisha maeneo ya ufugaji kunachangia kuhamahama kwa mifugo na kusababisha migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, uharibifu wa mazingira na ueneaji wa magonjwa ya mifugo;

(ii) Ukosefu wa soko la uhakika la mazao ya mifugo na uvuvi hususan maeneo ya vijijini;

(iii) Uwekezaji mdogo katika sekta za mifugo na uvuvi hasa katika usindikaji wa mazao ya mifugo na uvuvi na katika Bahari Kuu kunaathiri mchango wa sekta katika pato la Taifa;

(iv) Kutopatikana kwa mikopo ya kutosha na yenye masharti nafuu kwa wafugaji na wavuvi;

(v) Kuenea kwa magonjwa ya mifugo, hususan ya milipuko, yasiyo na mipaka na yaenezwayo na kupe na mbung'o;

(vi) Upungufu wa mbegu bora za mifugo na samaki, pembejeo na huduma hafifu ya uhimilishaji;

(vii) Uhaba wa Maafisa ugani wa mifugo na uvuvi ikilinganishwa na mahitaji;

(viii) Ushiriki mdogo wa wadau katika kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya samaki na mazao ya uvuvi;

(ix) Elimu duni ya ufugaji bora, ufugaji usio wa kibiashara na matumizi duni ya teknolojia za kisasa kwa wafugaji na wavuvi; na

(x) Kutopata fedha za kutosha na kwa wakati ili kutekeleza majukumu yaliyoainishwa kwenye mpango kazi.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na changamoto hizi, Wizara imetekeleza yafuatayo:-

(i) Wizara kuendelea kuhimiza Serikali kutenga fedha za kutosha ili kuweza kukidhi mahitaji ya sekta.

(ii) Kuhamasisha Sekta binafsi kuwekeza katika sekta za mifugo na uvuvi kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji. Aidha, vijitabu vyenye kuonyesha fursa za uwekezaji katika sekta za mifugo na uvuvi vimeandaliwa na kusambazwa kwa wadau na kutangazwa kwenye tovuti ya Wizara na kupitia ofisi za Ubalozi.

(iii) Kushirikiana na Mamlaka husika kuhimiza uainishaji, upimaji, umilikishaji na uendelezaji wa maeneo ya ufugaji ili yawe endelevu kwa lengo la kudhibiti uhamaji holela wa mifugo ili kupunguza migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi na hivyo kupunguza uharibifu wa mazingira na kuzuia kuenea kwa magonjwa ya mifugo. Aidha, Serikali imeanza

kupima upya baadhi ya ranchi zake kwa lengo la kupunguza migogoro kati ya ranchi na wafugaji.

(iv) Kuimarisha huduma za afya ya mifugo kwa kudhibiti magonjwa ya mifugo hususan ya milipuko ikiwa ni pamoja na kuendelea kutoa ruzuku ya madawa ya kuogeshea mifugo na chanjo. Aidha, Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) unaendelea kuimarishwa kwa ajili ya kuboresha huduma za kimaabara ikiwemo uzalishaji wa chanjo za mifugo.

(v) Kuhamasisha taasisi za fedha kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa ufugaji na uvuvi. Aidha, kuhamasisha wafugaji na wavuvi kuunda vyama vya ushirika vya akiba na mikopo ili kuwawezesha kupata pembejeo na zana kwa ajili ya ufugaji na uvuvi.

(vi) Kuendelea kuimarisha Wakala za Mafunzo ya Mifugo na Elimu na Mafunzo ya Uvuvi ili kuongeza udahili kutoka **2,451** hadi **2,500** (mifugo) na **1,180** hadi **1,500** (uvuvi) kuimarisha huduma za mafunzo na kuongeza idadi ya maafisa ugani wa

mifugo na uvuvi katika Halmashauri nchini. Aidha, kuendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika mafunzo ya mifugo na uvuvi. Hadi sasa, kuna vyuo **21** vya sekta binafsi ambavyo vimedahili wanafunzi **534**. Vilevile Wizara kuendelea kushawishi Serikali kuendelea kuajiri wataalam mbalimbali wa mifugo na uvuvi ili kukidhi mahitaji ya huduma za ugani.

(vii) Kuanzisha na kuimarisha vituo vya kuzalisha mbegu na pembejeo bora za mifugo na samaki pamoja na kuimarisha huduma ya uhimilishaji (artificial insemination); ufugaji wa samaki na ukuzaji wa viumbe wengine kwenye maji (aquaculture).

(viii) Kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi kuimarisha na kujenga miundombinu muhimu ya mifugo na uvuvi ikiwemo minada, masoko na mialo na kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kuongeza thamani ya mazao mifugo na uvuvi

(ix) Kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya uvuvi kwa kuhimiza na kuimarisha ushirikishwaji wa jamii na wadau wengine katika ulinzi,

usimamizi na matumizi endelevu ya raslimali za uvuvi. Aidha, vituo vya doria, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu (DSFA) na vikundi vya kusimamia rasilimali za uvuvi (BMUs) vinaimarishwa. Vilevile, Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu kitaimarishwa ili kiweze kuanzisha na kuendeleza maeneo tengefu kwenye maziwa makuu hususan Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa.

(x) Kuhimiza wafugaji na wavuvi kutumia kanuni bora za ufugaji na uvuvi kwa kutoa mafunzo kupitia vyombo vya habari, semina, shamba darasa, machapisho, na mafunzo mbalimbali. Aidha, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) zinaimarishwa ili kuendeleza huduma za utafiti wa mifugo na uvuvi ikiwa ni pamoja na kukarabati miundombinu, kuwajengea uwezo watafiti na kuwapatia vitendea kazi muhimu.

## 4.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA 2014/2015 NA MWELEKEO WA BAJETI YA MWAKA 2015/2016

### 4.1 Ukusanyaji wa Mapato

15. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara pamoja na Taasisi na Wakala chini yake ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi **24,401,371,000.00.** Kati ya hizo, shilingi **12,751,376,000.00 (52.3%)** ni kutoka Sekta ya Mifugo na shilingi **11,649,995,000.00 (47.7%)** ni kutoka Sekta ya Uvuvi. Hadi kufikia Aprili, 2015 kiasi cha shilingi **17,879,149,052.89** kimekusanywa na Wizara ikiwa ni sawa na asilimia **73** ya lengo la makusanyo**.** Kati ya hizo, shilingi **6,486,534,071.40** zimekusanywa kutoka sekta ya mifugo na shilingi **11,392,614,981.49** zimekusanywa kutoka sekta ya uvuvi. Katika mwaka 2015/2016, Wizara inatarajia kukusanya shilingi **43,862,624,975.00**. Kati ya hizo, shilingi **25,981,423,602.00** zitakusanywa na Wizara na shilingi **17,881,201,373.00** zitakusanywa na Taasisi, Wakala na Bodi zilizo chini ya Wizara ambazo zitatumiwa na Taasisi, Wakala na Bodi hizo kutekeleza majukumu yake.

## 4.2 Matumizi ya Fedha za Mwaka 2014/2015

16. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi imetengewa kutumia jumla ya shilingi **64,572,749,172.90.** Kati ya kiasi hiki, shilingi **39,820,344,172.90** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **24,752,405,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, shilingi **21,964,824,172.90** ni kwa ajili ya Matumizi Mengine (OC) na shilingi **17,855,520,000.90** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) ya watumishi wa Wizara. Vilevile, kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo, shilingi **22,529,800,000 (91%)** ni fedha za ndani na shilingi **2,222,605,000 (9%)** ni fedha za nje.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili 2015, jumla ya shilingi **29,797,977,826.00** zimetolewa, sawa na asilimia **74.83** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo, shilingi **17,696, 738,742** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara (PE) na shilingi **12,101,239,084.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengine (OC). Kati ya fedha hizo, jumla ya shilingi **29,724,815,596.41** asilimia **99.7** zimetumika. Aidha, jumla ya shilingi **3,934,042,500** (asilimia **15.9**) zimetolewa kwa ajili ya

kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo jumla ya shilingi **2,636,529,190.31** (asilimia **67.0**) zimetumika. Kati ya fedha za maendeleo zilizotolewa, shilingi **3,393,457,500** ni fedha za ndani na shilingi **540,585,000** ni fedha za nje.

### 4.3 Utekelezaji wa Sera, Programu na Sheria za Sekta

#### Sera na Programu za Sekta ya Mifugo

18. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 ambapo elimu ilitolewa kuhusu Sera hiyo kupitia matukio mbalimbali ya kitaifa yakiwemo, Sikukuu ya Wakulima Nanenane; Wiki ya Maziwa; Siku ya Chakula Duniani; Wiki ya Utumishi wa Umma, Siku ya Veterinary Duniani pamoja na mikutano mbalimbali ya kitaaluma na wadau. Vile vile Wizara iliendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo ya mwaka 2011 kupitia miradi mbalimbali. Katika kipindi hicho jumla ya nakala **300** za Sera, nakala **200** za Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo (2010) na nakala **300** za Programu ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo (2011) zilisambazwa. Aidha, Wizara inaendelea kushirikiana na Wizara za Sekta ya Kilimo katika maandalizi ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Nchini Awamu ya Pili na Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo.

**Sera na Programu za Sekta ya Uvuvi**

19. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Uvuvi na Mikakati yake ya mwaka 1997 na kuandaa Sera mpya ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 2014 ambayo imepitishwa na Baraza la Mawaziri. Vile vile, Wizara iliendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Uvuvi ya mwaka 2012 kupitia miradi mbalimbali ikiwa pamoja na kutoa elimu kupitia Sikukuu ya Wakulima Nanenane; Siku ya Chakula Duniani; Siku ya Uvuvi Duniani; Wiki ya Utumishi wa Umma pamoja na mikutano mbalimbali ya kitaaluma na wadau. Aidha, nakala **150** za Programu ya Kuendeleza Sekta ya Uvuvi na nakala **200** za Fursa za Uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi zilisambazwa kwa wadau.

**Sheria na Kanuni za Sekta za Mifugo na Uvuvi**

20. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuboresha Sheria na Kanuni za Sekta za Mifugo na Uvuvi kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuandaa na kupitishwa na Baraza la Mawaziri Waraka wa Mapendekezo ya Sheria mpya ya Taasisi ya Utafiti

wa Uvuvi Tanzania (The Tanzania Fisheries Research Institute Act) na Muswada wa Sheria utawasilishwa Bungeni;

(ii) Kuandaa mapendekezo ya kutunga Sheria mpya ya Mamlaka ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu ambayo yapo katika ngazi ya Makatibu Wakuu;

(iii) Kuandaa mapendekezo ya kutunga Sheria mpya ya Mbari Bora za Wanyama (Animal Breeding Act) ambayo ipo katika hatua ya kujadiliwa na wadau;

(iv) Kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu (The Deep Sea Fishing Authority Act) SURA 388 kwa ajili ya kupata maoni ya wadau;

(v) Kufanya mikutano ya wadau wa sekta ya uvuvi ili kuainisha maeneo yanayohitaji marekebisho katika Sheria ya Uvuvi (The Fisheries Act) SURA 279;

(vi) Kuandaa Waraka wa Taarifa ya Utekelezaji wa Maamuzi ya Baraza la Mawaziri katika Waraka Na. 2/2002

kuhusu Mapendekezo ya Mkakati wa Ubinafsishaji wa Mashamba ya Mifugo na Ranchi za Taifa na kujadiliwa katika ngazi ya Makatibu Wakuu;

(vii) Kuandaa Waraka wa Taarifa ya Utekelezaji wa Maamuzi ya Baraza la Mawaziri katika Waraka Na. 6/2000 kuhusu Ubinafsishaji wa Kiwanda cha Kusindika Nyama cha Tanganyika Packers Limited (TPL) - Mbeya ambao upo katika ngazi ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri; na

(viii) Kutafsiri Sheria ya Nyama SURA 421 katika lugha ya Kiswahili.

Aidha, Kanuni zifuatazo zimeandaliwa na kupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kutangazwa katika Gazeti la Serikali:

(i) Kanuni za Veterinari 'The *Veterinary (Recognition of* Livestock *Training Institutes and Companies Undertaking Veterinary Practice Regulations', 2014,* Tangazo la Serikali Na. 486 la mwaka 2014; na

(ii) Kanuni za Uvuvi *"The Fisheries (Amendment) Regulations, 2014,*

Tangazo la Serikali Na.10 la mwaka 2015.

Pia, Wizara imekamilisha uchapaji wa Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009, Tangazo la Serikali Na. 308 la mwaka 2009 zilizotafsiriwa katika lugha ya Kiswahili baada ya kuwa zimeidhinishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ilifanya kikao mjini Dodoma kwa lengo la kutoa elimu kuhusu dhana ya ugatuaji madaraka (D by D) na kujadili kwa kina changamoto zilizopo na kuweka mikakati ya kuboresha sekta za mifugo na uvuvi.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kutoa elimu kuhusu Sera, Sheria na Kanuni za sekta za mifugo na uvuvi ili zizingatie mfumo wa ugatuaji madaraka (D by D). Pia, itachapisha na kusambaza nakala **300** za Sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 2014 na kukamilisha Mkakati wa kutekeleza Sera hiyo. Aidha, Wizara itakamilisha kuandaa mapendekezo ya kutunga Sheria mpya ya Mamlaka ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu; Sheria ya Mbari Bora za Wanyama (Animal Breeding Act); Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu (The Deep Sea Fishing Authority Act); Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania na Sheria ya Uvuvi (The Fisheries Act).

## 4.4 Uendelezaji wa Sekta ya Mifugo

### Uzalishaji na Biashara ya Mifugo na Mazao yake

### Zao la Maziwa

22. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 Wizara iliendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji na usindikaji wa maziwa ambapo uzalishaji wa maziwa umeongezeka kwa **asilimia 3.5** kutoka lita **bilioni 1.99** mwaka 2013/2014 hadi kufikia lita **bilioni 2.06** mwaka 2014/2015**.** Aidha, kiasi cha maziwa kinachosindikwa kwa siku kimeongezeka kutoka **lita 139,800** mwaka 2013/2014 hadi **lita 167,070** mwaka 2014/2015 kwa mwaka sawa na ongezeko la asilimia **19.5.** Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa viwanda vya kusindika maziwa kutoka **74** mwaka 2013/14 na kufikia **82** mwaka 2014/2015 **(Jedwali Na. 1).**

23. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara iliratibu Programu ya Unywaji Maziwa Shuleni ambayo ilifanyika mkoani Kilimanjaro na kushirikisha shule **18.** Idadi ya wanafunzi wanaopata maziwa nchini ni **14,788** ambao wanatumia lita **7,394** za maziwa**,** sawa na wastani wa nusu lita kwa wiki kwa mtoto. Aidha, uanzishwaji wa Programu ya Unywaji Maziwa Shuleni (School Milk Feeding

Program - SMFP) umeanza katika shule **10** zilizopo katika wilaya ya Kinondoni. Vilevile, Wizara imesajili wadau **144** kati ya hao, **53** wazalishaji wa maziwa, **36** wafanyabiashara wa maziwa na **15** waingizaji wa maziwa kutoka nje, **21** vioski vya maziwa/maduka makubwa, wanne (**4**) wasindikaji wa maziwa na **15** vituo vya kukusanyia maziwa. Pamoja na usajili wa wadau Bodi ya Maziwa Tanzania iliweza kutoa vibali kwa magari **182** ya kusafirishia maziwa.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuhamasisha ukusanyaji na usindikaji wa maziwa ili kuongeza usindikaji kufikia lita **230,000** kwa siku.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kukarabati mashamba ya kuzalisha mitamba, kupima mashamba na kuyapatia vitendea kazi ili yaweze kuzalisha kwa urahisi. Katika mwaka 2014/15 Wizara ilitekeleza yafuatayo:-

(i) Kuzalisha na kusambaza jumla ya mitamba 635 kwa wafugaji wadogo;

(ii) Kununua ng'ombe wazazi **75** kwa ajili ya mashamba ya Ngerengere (**30)** na Mabuki (**45)**;

(iii) Kujenga ofisi katika shamba la uzalishaji mitamba Mabuki;

(iv) Kukarabati mashine ya kukamulia maziwa na ununuzi wa mbegu za malisho kwa ajili ya shamba la uzalishaji mitamba Kitulo;

(v) Kuendeleza malisho hekta **172,** katika mashamba ya Ngerengere (**35**), Nangaramo (12), Mabuki (**20**), Sao Hill (**40**) na Kitulo (**100**);

(vi) Kuweka makinga moto na uzio kilometa **43**. kwenye maeneo ya malisho katika mashamba yote ya kuzalisha mitamba ya Kitulo (**25**), Ngerengere (**5**) Sao Hill **(5**), na Nangaramo (**8**);

(vii) Kupima shamba la mitamba la Nangaramo na kupatiwa hati miliki Na. 427636 NANY/LD/413 shamba Na. 189; na

(viii) Kukarabati lambo kwa ajili ya maji ya mifugo katika shamba la uzalishaji mitamba Nangaramo.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) imezalisha mitamba **638** na Mashirika yasiyo ya Kiserikali ilisambaza jumla ya mitamba **10,731** kwa

wafugaji wadogo katika mikoa **25** nchini (**Jedwali Na. 2a na Na. 2b).**

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuimarisha mashamba ya kuzalisha mitamba matano (**5)**, kununua ng'ombe wazazi **250** kwa ajili ya mashamba ya kuzalisha mitamba ya Mabuki (**50**), Nangaramo (**50**), Sao Hill (**50**), Kitulo (**50**) na Ngerengere (**50**), kukarabati nyumba za watumishi wa shamba la Kitulo na Ngerengere na kuweka makinga moto na uzio kilometa **50** katika mashamba matano (**5)** ya kuzalisha mitamba.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** uhimilishaji ni teknolojia mojawapo inayotumika kuongeza ubora wa mifugo. Katika mwaka 2014/2015 Wizara imeendelea kuratibu na kuhamasisha matumizi ya teknolojia hiyo kwa kuimarisha na kuongeza vituo vya uhimilishaji kwa kufanya kazi zifuatazo:-

(i) Kuimarisha kituo cha Taifa cha Uhimilishaji – NAIC Usa River kwa kukinunulia vitendea kazi mbalimbali vikiwemo vifaa vya maabara na uhimilishaji;

(ii) Kukamilisha ujenzi wa kituo kipya cha Katavi na hivyo kuwa na vituo **sita** (**6**) vya kanda vya huduma za

usambazaji wa mbegu na uzalishaji wa kimiminika cha naitrojeni ambavyo ni Mbeya, Mwanza, Pwani, Dodoma, Lindi na Katavi;

(iii) Kuendeleza ujenzi na kusimikwa mtambo wa kuzalisha kimiminika cha naitrojeni na kujenga mabanda **7** ya madume bora katika Kituo cha Uhimilishaji cha Sao Hill;

(iv) Kuhimilisha ng’ombe **105,000** ikiwa ni ongezeko la asilimia **14.5** ikilinganishwa na mwaka 2013/2014;

(v) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wahimilishaji **181** kuhusu matumizi sahihi ya teknolojia ya uhimilishaji katika kituo cha uhimilishaji cha Taifa (NAIC) Usa River;

(vi) Kukarabati mitambo ya kuzalishia liquid Nitrogen ya Lindi, Mwanza na Uyole; na

(vii) Kuzalisha dozi **70,294** za mbegu bora za uhimilishaji na kusambazwa kwa wafugaji.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuimarisha kituo cha Taifa cha uhimilishaji

NAIC Usa River na vituo sita (**6**) vya uhimilishaji vya Kanda ili kuwa na ufugaji wenye tija nchini.

**Tasnia ya Nyama: Ng'ombe, Mbuzi, Kondoo, Nguruwe na Kuku**

26. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushirikiana na wadau wa nyama kuendeleza sekta ndogo ya nyama ambayo inahusisha ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku. Katika mwaka 2014/2015 uzalishaji wa nyama umeongezeka kwa **asilimia 6.2** kutoka tani **563,086** mwaka 2013/2014 hadi tani **597,757** mwaka 2014/2015 (**Jedwali Na. 3**). Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyama katika soko maalum la ndani hususan migodi, maduka makubwa na hoteli za kitalii. Aidha, idadi ya ngómbe walionenepeshwa waliongezeka kutoka ng'ombe **175,000** mwaka 2013/2014 hadi **213,000** mwaka 2014/2015 (**Jedwali Na. 4).**

27. ***Mheshimiwa Spika,*** miundombinu ya masoko ya mifugo imeendelea kuboreshwa kwa lengo la kukuza biashara ya mifugo katika minada ya upili na mipakani. Katika kipindi cha mwaka 2014/2015, minada ya Pugu (Ilala), Lumecha (Songea), Kirumi (Butiama) na Nyamatala (Misungwi) imekarabatiwa. Aidha, Wizara imetengeneza barabara kuzunguka

mnada wa upili wa Kizota (Dodoma), kukarabati nyumba za watumishi na kurudishia mawe ya mipaka. Pia, Wizara imejenga ofisi, mazizi na barabara ya kuingilia mnadani, sehemu ya kunadia mifugo katika mnada wa upili wa Kasesya (Kalambo). Vilevile, usimikaji wa mizani ya mifugo katika minada ya upili **11** na uhamasishaji juu ya matumizi yake umefanyika.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itajenga minada miwili ya upili ya Longido (Longido) na Kirumi (Butiama) na kukarabati minada **7** ya mifugo ya upili ya Weruweru (Hai), Meserani (Monduli), Themi (Arusha), Sekenke (Iramba), Igunga (Igunga), Ipuli (Tabora) na Mhunze (Kishapu), kutoa mafunzo kwa wakusanyaji maduhuli **60** na wafanyabiashara wa mifugo **400** ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato na soko la mifugo. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu uuzaji wa mifugo katika minada ya awali, upili na mipakani na kuhamasisha matumizi ya mizani ya kupimia uzito wa mifugo.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, jumla ya ng'ombe **1,337,095** mbuzi **1,056,218** na kondoo **230,221** wenye thamani ya shilingi **bilioni 1,027.4** waliuzwa minadani ikilinganishwa na ng'ombe **1,215,541**, mbuzi **960,199** na kondoo **209,292** wenye thamani ya shilingi **bilioni 989.3** mwaka 2013/2014. Pia, idadi ya mifugo iliyouzwa nje ya nchi

imeongezeka kutoka ng'ombe **1,123** mwaka 2013/2014, hadi ng'ombe **2,139** wenye thamani ya shilingi **bilioni 34** mwaka 2014/2015. Aidha, jumla ya **tani 23.4** za nyama ya ng'ombe, nyama ya mbuzi **tani 1,388.9** na nyama ya kondoo **tani 36.7** zenye thamani ya shilingi **bilioni 52.1** ziliuzwa katika nchi za Msumbiji, Vietnam, Oman, Qatar na Falme za Kiarabu. Vilevile, jumla ya tani **735** za nyama ya ng'ombe, tani **804** za nyama ya nguruwe na tani **16.5** za nyama ya kondoo ziliingizwa nchini.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuhamasisha wadau kuwekeza katika ujenzi wa viwanda na biashara ya mifugo na mazao yake ili kuongeza mauzo ya nyama ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuhamasisha wafugaji na wafanyabiashara ya mifugo kuwekeza katika ufugaji wa kisasa ukiwemo wa ranchi na unenepeshaji. Vilevile, Wizara itaendelea kuhamasisha unenepeshaji ili kufikia idadi ya ng'ombe **300,000** kwa mwaka.

**Uzalishaji wa Nyama katika Kampuni ya Ranchi za Taifa (National Ranching Company - NARCO)**

29. ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) inayomiliki ranchi kumi (**10**) za mfano za Kagoma, Kalambo, Kikulula,

Kongwa, Mabale, Missenyi, Mkata, Mzeri, Ruvu na West Kilimanjaro ina jumla ya hekta **230,384** zenye uwezo wa kuweka ng'ombe kati ya **80,000** na **90,000**. Kwa sasa, Kampuni ina jumla ya ng'ombe **12**,**681,** kondoo na mbuzi **2,166**, farasi **39** na punda **15.** Katika mwaka 2014/2015, NARCO imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuzalisha ndama **3,045** kutokana na ng'ombe wazazi **5,786**;

(ii) Kunenepesha ng'ombe **2,100** kutoka kwa wafugaji na kuuza ng'ombe **4,900** wenye thamani ya shilingi **bilioni 2.7**;

(iii) Kutoa ushauri na mafunzo ya kusimamia ufugaji wa kisasa kwa wawekezaji watanzania **100** ambao wamemilikishwa vitalu ndani ya Ranchi za Taifa pamoja na wafugaji wanaozunguka ranchi hizo. Vitalu hivyo vimewekeza ng'ombe **31,600**, kondoo na mbuzi **8,200**;

(iv) Kukamilisha majadiliano na Kampuni ya Allanasons kutoka India kwa ajili ya uwekezaji katika machinjio ya kisasa katika ranchi ya Ruvu kwa ajili ya soko la nje. Machinjio hii itakapokamilika

itakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe **1,000** kwa siku;

(v) Kufungua vituo vipya viwili vya mauzo ya nyama ya ***Kongwa beef*** katika mikoa ya Dodoma (Kibaigwa) na Tanga (Mombo);na

(vi) Kununua ng'ombe wazazi **1,200** ili kuongeza idadi ya ng'ombe katika ranchi zake.

Katika mwaka 2015/2016, NARCO inatarajia kuzalisha jumla ya ndama **3,366** kutokana na ng'ombe wazazi **4,488,** kuendelea na ujenzi wa machinjio ya kisasa ya Ruvu na kununua ng'ombe wazazi **1,200** kwa lengo la kuongeza idadi ya ng'ombe katika ranchi zake. Aidha, Kampuni itaendelea kuongeza uzalishaji kwa kutafuta mitaji mipya na kuvutia wawekezaji kwa ubia katika ranchi zake.

**Kuku**

30. ***Mheshimiwa Spika,*** ufugaji wa kuku nchini umeendelea kukua, ambapo katika mwaka 2014/2015, uzalishaji wa vifaranga vya kuku wa nyama na mayai umeongezeka na kufikia vifaranga **milioni 63.6** ikilinganishwa na vifaranga **milioni 61** vilivyozalishwa mwaka 2013/2014. Aidha, jumla ya mayai ya kutotolesha vifaranga **1,750,000** yaliingizwa

nchini kutoka nchi za Malawi, Hungary, Uholanzi, Kenya, Ufaransa, Afrika ya Kusini, Hispania, Ubelgiji, Uingereza, Zambia na Mauritius kwa ajili ya kutotolesha vifaranga vya kuku wazazi. Vilevile, uzalishaji wa mayai umeendelea kuongezeka kutoka **bilioni 3.9** mwaka 2013/2014 hadi mayai **bilioni 4.15** mwaka 2014/2015.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuhamasisha utekelezaji wa programu za kuendeleza mifugo midogo ikiwemo kuku wa asili, kuku wa kisasa na kware katika Mamlaka za Serikali za Mitaa **20** za Mikoa ya Singida, Mwanza, Tabora, Kagera, Morogoro, Mtwara, Simiyu na Lindi.

**Nguruwe**

31. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara iliendelea kuimarisha uzalishaji wa nguruwe nchini kwa kuendeleza shamba la Ngerengere kwa kuwapatia nguruwe wazazi **10**. Aidha, uzalishaji wa nyama ya nguruwe umeongezeka kutoka tani **79,174** hadi kufikia tani **79,180** mwaka 2014/2015. Pia, Wizara kwa kushirikana na Mamlaka za Serikali za Mitaa imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ufugaji wa nguruwe wa kisasa.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuimarisha shamba la mifugo la Ngerengere ili liweze kuzalisha na kusambaza mbegu bora za nguruwe kwa wafugaji kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa nguruwe na nyama yake. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa nguruwe.

**Ngozi**

32. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 kumekuwa na ongezeko la ngozi zilizosindikwa kutoka vipande vya ngozi za ng'ombe **1,060,777** na vipande vya mbuzi na kondoo **2,715,436** mwaka 2013/2014 hadi vipande vya ngómbe **1,388,139** na vipande vya mbuzi na kondoo vimepungua kutoka vipande **2,715,436** mwaka 2013/2014 hadi kufikia vipande **1,020,000** kwa mwaka 2014/2015 vyenye thamani ya shilingi **bilioni 39.2.** Ongezeko hili limetokana na ukuaji wa usindikaji katika kiwanda cha SAK International Ltd – Arusha (vipande **1,055,000**) na kuanza usindikaji katika viwanda vipya vya ngozi vya Meru Tannery-Arusha (vipande **856,000)** na Xing Hua Investment Tannery-Shinyanga (vipande **770,000**). Pia, ongezeko hilo limetokana na mikataba ya usindikaji wa ngozi iliyofanywa na wafanyabiashara wasio na viwanda katika kiwanda cha ngozi Morogoro.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia na kutekeleza Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi Nchini kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Wizara ya Viwanda na Biashara, Mamlaka za Serikali za Mitaa **75** na Chama cha Wadau wa Ngozi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo (*Livestock Development Fund*) kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuhamasisha matumizi ya mfumo wa ufuatiliaji wa uzalishaji na biashara ya ngozi kutoka machinjioni hadi viwandani ili kuzuia utoroshaji wa ngozi nje ya nchi katika mikoa ya Kanda ya Ziwa kwa kutoa mafunzo kwa vyombo vya ulinzi na usalama **(58**); maafisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (**29**); na maafisa ngozi na maafisa mifugo (**29**) maafisa biashara (**29**); wafanyabishara wa ngozi (**29**) na wachinjaji (**29**);

(ii) Kuwezesha vikao sita (**6**) vya kisheria vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Ngozi na Kamati ya Usimamizi wa Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo; na

(iii) Kuwajengea uwezo wataalam **130** kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa **65** ambazo haziko kwenye mpango wa kutekeleza Mkakati wa Kufufua na

Kuendeleza Sekta ya Viwanda vya Ngozi kuhusu uzalishaji, uhifadhi na usindikaji wa ngozi unaozingatia hifadhi ya mazingira.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati huo kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuwezesha mafunzo kwa wataalam wa mifugo katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa **75** kuhusu uendelezaji wa zao la ngozi nchini;

(ii) Kufuatilia na kutathimini utekelezaji wa kazi za Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi;

(iii) Kuendelea kuhamasisha matumizi ya mfumo wa ufuatiliaji wa uzalishaji na biashara ya ngozi kutoka machinjioni hadi viwandani ili kuzuia utoroshwaji wa ngozi nje ya nchi;

(iv) Kuwezesha uendeshaji wa vikao vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Ngozi na Kamati ya Usimamizi wa Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo ili kutekeleza majukumu yake; na

(v) Kuwezesha wadau kushiriki katika biashara ya ngozi ya ndani na nje ya nchi kwa kuwawezesha kushiriki katika maonesho ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

**Matumizi ya Rasilimali za Ardhi, Maji na Malisho kwa Mifugo na Utatuzi wa Migogoro**

34. ***Mheshimiwa Spika,*** uendelezaji wa ufugaji wa asili unahitaji kutenga maeneo ya malisho, kuyaendeleza na kuyasimamia ikiwa ni pamoja na kutathmini uwezo wake na kuyawekea miundombinu muhimu. Katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na TAMISEMI zimetenga maeneo ya malisho na kufanya eneo lililotengwa kwa ajili hiyo kufikia hekta **milioni 1.95** katika vijiji **620** katika Mamlaka za Serikali za Mitaa **81** zilizopo katika mikoa **22** (**Jedwali Na. 5**).

Katika mwaka 2015/2016, Wizara kwa kushirikana na wadau itawezesha kutambua na kutenga maeneo ya malisho kwa ajili ya ufugaji endelevu katika wilaya za Busega, Kiteto, Kilosa, Ngorongoro, Mvomero, Kilindi, Igunga, Iramba na Lindi. Aidha, ili kupunguza uvamizi wa mashamba ya Serikali, Wizara itawezesha utambuzi na upimaji wa mipaka ya maeneo ya mashamba manne (**4)** ya kuzalisha mitamba, mawili (**2**) ya mbegu bora za malisho, minada **12**

ya upili na Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji cha NAIC Usa River.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuboresha mashamba ya uzalishaji wa mbegu bora za malisho ya Vikuge (Pwani), Langwira (Mbeya), Sao Hill (Iringa), Mabuki (Mwanza), LRC Tanga (Tanga), Kizota na PRC Kongwa (Dodoma) kwa kukarabati miundombinu na kuyapatia vitendea kazi. Katika mwaka 2014/2015, jumla ya tani **48.5** za mbegu za malisho zilizalishwa ikilinganishwa na tani **48.2** za mwaka 2013/2014. Pia, uzalishaji wa hei umeongezeka kutoka marobota **922,620** kutoka mashamba ya Serikali na sekta binafsi mwaka 2013/2014 hadi marobota ya hei **1,098,311** mwaka 2014/2015. Kati ya hayo, marobota **499,820** yamezalishwa kutoka katika mashamba ya Serikali na **598**,**491** kutoka sekta binafsi (**Jedwali Na. 6a** na **6b**).

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuimarisha mashamba ya kuzalisha mbegu bora za malisho ya Vikuge, Langwira, Sao Hill, Kizota na Mabuki, kwa kuyanunulia vitendea kazi na kuboresha miundombinu ya shamba na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa malisho na mbegu bora za malisho.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15 Wizara imeendelea kusimamia ujenzi Mabwawa matatu (**3**) ya Kwamaligwa (Kilindi), Mbangala (Chunya) na Olypasei (Kiteto) yanajengwa na Wakala wa Kuchimba Visima Virefu na Malambo (Drilling and Dam Construction Agency-DDCA) ambapo Mkandarasi ameshakabidhiwa maeneo na utekelezaji umeshaanza.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika; Wizara ya Mambo ya Ndani na wadau mbalimbali ilifanya mkutano Mwanza kujadili changamoto na njia mbalimbali za kutatua migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Katika mwaka 2015/2016 Wizara itawezesha ujenzi wa malambo katika wilaya za Chemba, Mwanga, Tarime, Bagamoyo, Busega, Kishapu, Kilwa na Ngorongoro na itakamilisha ujenzi wa kisima kirefu katika Halmashauri ya Wilaya ya Same.

## Usindikaji wa Vyakula vya Mifugo

38. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 Wizara imeendelea kuratibu

usindikaji na kusimamia ubora wa vyakula vya mifugo vinavyozalishwa na sekta binafsi ambayo imezalisha jumla ya tani **1,200,000** za vyakula vya mifugo kutoka katika viwanda **80.** Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa wakaguzi wa vyakula vya mifugo **159** kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa **25** katika mikoa nane **(8)** ya Mtwara, Pwani, Mbeya, Morogoro, Dodoma, Iringa, Dar es Salaam na Njombe ili kuwajengea uwezo wa kudhibiti ubora wa vyakula vya mifugo.

Katika mwaka 2015/2016 Wizara itawajengea uwezo Wakaguzi **128** kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu ukaguzi na udhibiti wa ubora wa vyakula vya mifugo. Aidha, Wizara itaendelea kuwaelekeza wadau kusajili maeneo ya uzalishaji na uhifadhi wa vyakula vya mifugo kupitia tovuti ya Wizara ambayo ni www.mifugouvuvi.go.tz

## 4.5 Udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo

### Kuimarisha Maeneo Huru ya Magonjwa ya Mifugo

39. ***Mheshimiwa Spika,*** biashara ya mifugo na mazao yake katika soko la ndani na nje inapasa kuzingatia viwango vya ubora na usalama kwa walaji. Ili kukidhi vigezo vilivyowekwa na OIE na WTO, nchi husika ni lazima idhibiti magonjwa yanayoathiri mifugo

kwa kuwa na maeneo huru ya magonjwa ya mifugo. Katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kuendeleza eneo huru la magonjwa ya mifugo la Uwanda wa Juu wa Ufipa (Ufipa Plateau) kwa kuimarisha Kituo cha Ufuatiliaji na Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo cha Kanda ya Kusini Magharibi kilichopo mjini Sumbawanga kwa kukarabati ofisi, kuongeza mtaalam wa magonjwa ya mifugo na kumjengea uwezo mtaalam huyo juu ya utambuzi wa magonjwa ya mlipuko kwa kuzingatia kanuni za biashara za mifugo na mazao yake kitaifa na kimataifa.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuimarisha Eneo huru la Magonjwa ya Mifugo la Uwanda wa Juu wa Ufipa (Ufipa Plateau) ulio katika wilaya za Kalambo, Nkasi na Sumbawanga kwa kuhamasisha na kutoa mafunzo kwa wafugaji na wadau waliopo kwenye eneo hilo ili kuongeza kiwango cha ushiriki wao kwenye shughuli za kukinga magonjwa na kuzalisha kibiashara. Aidha, kuendelea na taratibu za kuzifanya ranchi za Ruvu na Kongwa kuwa maeneo huru ya magonjwa ya mifugo ili kuwezesha viwanda na machinjio za kisasa zinazojengwa katika maeneo hayo kuweza kuuza nyama nje ya nchi.

## Magonjwa ya Mlipuko

### (i) Sotoka ya Mbuzi na Kondoo

40. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana, Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau iliendelea kudhibiti ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Mara na Pwani kwa kuchanja mbuzi na kondoo **638,007** na kutoa elimu kwa wafugaji. Matukio ya ugonjwa huu yanaendelea kupungua katika mikoa husika.

Katika mwaka 2015/2016 Wizara itaendelea kuzuia na kudhibiti kuenea kwa ugonjwa huu kwa kuratibu, kununua na kusambaza dozi **1,000,000** za chanjo zitakazotumika katika wilaya zilizo katika hatari ya kuambukizwa ugonjwa kutokana na taarifa za kiepidemiolojia zitakavyokuwa zinatolewa. **(Kiambatisho Na. 1**).

### (ii) Homa ya Mapafu ya Ng'ombe

41. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kudhibiti Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP) kwa kufuatilia ugonjwa huo katika maeneo ya mikoa ya Arusha, Kigoma, Manyara, Pwani, Rukwa na Tanga yaliyoonekana kuwa ni chanzo cha maambukizi. Aidha, Wizara

imeendelea kusimamia usafirishaji wa mifugo nchini na kusambaza dozi **120,000** za chanjo.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuratibu shughuli za udhibiti wa ugonjwa wa Homa ya Mapafu kwa kununua na kusambaza chanjo kutegemea mwenendo wa ugonjwa na upatikanaji wa fedha.

### (iii) Mafua Makali ya Ndege

42. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kufuatilia mwenendo wa Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege (HPAI) hapa nchini na nje ya nchi. Taarifa ya ufuatiliaji inaonesha nchi **13** zina ugonjwa huu, hivyo uwezekano wa ugonjwa huu kuingia nchini bado ni mkubwa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine kama Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO), Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE), imechukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huu kwa kutoa mafunzo ya utambuzi na ufuatiliaji kwa wataalam **3** wa maabara na mtaalamu mmoja wa epidemiolojia.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine, itaendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa

huu kwa kufuatilia mwenendo wa ugonjwa ndani na nje ya nchi.

**Magonjwa yaenezwayo na Kupe na Mbung'o**

(i) **Udhibiti wa Kupe na Magonjwa wayaenezayo**

43. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2014/2015 Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta binafsi imeendelea kutekeleza mpango wa ruzuku ya asilimia **40** kwa dawa za kuogesha mifugo ambapo lita **119,509** zenye kiini cha pareto na *amitraz* zilinunuliwa kwa thamani ya shilingi **1,817,911,200** na kusambazwa katika Mikoa **21** ya Tanzania Bara. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi imechanja ng'ombe **19,491** dhidi ya Ndigana kali katika mikoa ikiwemo Arusha, Dar es Salaam, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Morogoro, Mbeya, Pwani na Tanga.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine itaendelea na utaratibu wa ruzuku ya dawa za kuogesha mifugo ambapo itanunua jumla ya lita **200,000** za viini vya pareto na *amitraz* zitakazotumika kuogesha mifugo **8,000,000.** Aidha, Wizara itaendelea kuratibu na kutoa miongozo kwa Mamlaka za

Serikali za Mitaa na wadau kuhusu ujenzi, ukarabati na uendeshaji wa majosho.

### (ii) **Udhibiti wa Mbung'o na Nagana**

44. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa udhibiti shirikishi na endelevu wa mbung'o kwa kutoa ushauri wa kitaalamu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nane **(8)** za Kilosa, Kisarawe, Monduli, Mpanda, Ngorongoro, Uvinza, Urambo na Serengeti. Aidha, udhibiti wa mbung'o katika ikolojia za Katavi, Serengeti, Kigoma, Tabora na Rukwa umeendelea kufanyika.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara kwa kupitia Programu ya Umoja wa Afrika wa Kuangamiza Mbung'o na Ndorobo "Pan African Tsetse and Trypanosomiasis Eradication Campaign (PATTEC)" itatekeleza Mkakati wa Kudhibiti Mbung'o na Ndorobo kwa kununua vitendea kazi na kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu mbinu shirikishi na endelevu katika mikoa ya Dodoma, Kagera, Katavi, Kigoma, Kilimanjaro, Mara, Pwani, Rukwa, Singida, Tabora na Tanga.

**Magonjwa ya Mifugo yanayoambukiza Binadamu**

(i) **Kichaa cha Mbwa**

45. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara kupitia Mradi wa Kutokomeza Kichaa cha Mbwa unaofadhiliwa na Taasisi ya *Bill & Melinda Gates Foundation* na kuratibiwa na Shirika la Afya Duniani imeendelea kudhibiti Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani, Morogoro na Dar es Salaam kwa njia ya kampeni; ambapo mbwa **81,830** na paka **15,999** walichanjwa sawa na asilimia **79** ya waliolengwa kuchanjwa. Aidha, elimu kuhusu ugonjwa huu na namna ya kujikinga iliendelea kutolewa kwenye maonyesho ya Nanenane na Siku ya Kichaa cha Mbwa Duniani.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kutoa elimu na kusambaza chanjo ya kichaa cha mbwa dozi **110,000** katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa za Pwani, Lindi na Mtwara.

(ii) **Homa ya Bonde la Ufa**

46. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara ilifuatilia viashiria na mwenendo wa ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa ambapo kwa taarifa kutoka taasisi za kimataifa za "National Aeronautics and Space Administration (**NASA**)", Shirika la Afya ya

Wanyama Duniani (OIE) na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) ilionesha hatari ya kuwepo kwa mlipuko katika msimu huu wa mvua. Kwa taarifa hiyo Wizara imenunua na kusambaza dozi **163,000** za chanjo ya Homa ya Bonde la Ufa kwa ajili ya kuchanja ng'ombe, kondoo na mbuzi kwenye maeneo hatarishi ya mikoa ya Dodoma, Arusha, Manyara, Kagera, Simiyu, Geita, Mara, Mwanza na Shinyanga. Aidha, elimu kuhusu udhibiti wa Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa ulitolewa katika maonesho ya NaneNane ambapo jumla ya vipeperushi **1,500** vilisambazwa.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Wizara za Afya na Ustawi wa Jamii, Maliasili na Utalii, na wadau wa kimataifa wakiwemo WHO, NASA, OIE, FAO itaendelea kufuatilia mwenendo wa ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa na kuchukua tahadhari stahiki. Aidha, Wizara itanunua dozi **163,000** za chanjo Homa ya Bonde la Ufa ili kudhibiti ugonjwa huo.

(iii) **Ugonjwa wa Kutupa Mimba (Brucellosis)**

47. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015, jumla ya ng'ombe **6,306** mbuzi **120,** kondoo na **80** walipimwa ugonjwa wa kutupa mimba katika Wilaya za Bagamoyo, Kyela, Korogwe, Lushoto na Njombe ambapo ng'ombe **118** na mbuzi **6** walithibitika kuwa na

ugonjwa huo na hatua stahiki zilichukuliwa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilitoa elimu kwa umma kuhusu Ugonjwa wa Kutupa Mimba ikiwemo jinsi ya kuutambua, madhara yake na kujikinga kupitia mikutano ya hadhara na maonesho mbalimbali ya Kitaifa.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea kufuatilia, kuchunguza na kutoa elimu na ushauri wa kitaalam katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara ili kudhibiti Ugonjwa wa Kutupa Mimba. Aidha, jumla ya sampuli **6,000** za damu zitachukuliwa na kuchunguzwa.

**Usalama wa Chakula kitokanacho na mifugo**

48. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi imetoa mafunzo kwa wafugaji **617** kuhusu mbinu bora za uzalishaji na matumizi sahihi ya dawa, chanjo, viuatilifu na kemikali za kuua vimelea (Disinfectants) ili kuzalisha mazao yenye ubora na salama. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Sekretariati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imeanza kuandaa Mpango wa Kudhibiti Sumu-kuvu (aflatoxins) kwenye vyakula vya mifugo kama pumba za mahindi, mashudu ya alizeti na pamba ili kuepusha

mazao yatokanayo na mifugo hususan maziwa na nyama.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi itaendelea kutoa mafunzo ya uzalishaji na matumizi sahihi ya pembejeo za mifugo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kilimo, Chakula na Ushirika na Mamlaka za Serikali za Mitaa, itatoa elimu ya mbinu za kuepuka sumu-kuvu kwenye mazao yanayotumika katika utengenezaji wa vyakula vya mifugo.

**Ukaguzi wa Mifugo na Mazao yake**

49. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kukagua mifugo na mazao yake ili kulinda afya ya wanyama na jamii. Ukaguzi huo umefanyika katika machinjio mbalimbali hapa nchini ambapo jumla ya ng'ombe **406,238,** mbuzi **203,270**, kondoo **66,113**, kuku **1,723,582** na nguruwe **20,088** walikaguliwa kwa ajili ya soko la ndani ya nchi. Aidha, jumla ya ng'ombe **1,013,** mbuzi **1,118** na kondoo **95** walikaguliwa na kuuzwa nje ya nchi wakiwa hai. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na FAO imetoa mafunzo kwa wakaguzi **10** wa nyama kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa yanayohusu usalama wa chakula kitokanacho na mifugo.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kusimamia na kufuatilia usalama wa chakula ili kulinda afya za walaji wa mazao ya mifugo na kukuza biashara ya mazao ya mifugo kimataifa.

**Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo**

50. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na FAO ilikamilisha ujenzi na kuzindua Kanzidata (Mfumo wa Utambuzi wa Ki – elekroniki) ya Utambuzi na Ufuatiliaji wa Mifugo (TANLITS) na kutoa mafunzo kwa wataalamu wa mifugo **75.** Aidha, Wizara iliwezesha utambuzi wa mifugo **45,000** katika makundi ya wafugaji wa ng’ombe wa asili ambapo jumla ya ng’ombe **13,054** wametambuliwa kwa njia ya hereni katika Wilaya za Bagamoyo, Muheza na Kibaha na ng’ombe **120,000** kwa njia ya chapa katika Wilaya za Karagwe na Morogoro. Aidha, mafunzo ya utekelezaji wa mfumo wa Utambuzi na Ufuatiliaji mifugo yalitolewa kwa wadau **98** kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa **30.** Vilevile, uhamasishaji wa umma kuhusu mfumo wa TANLITS ulifanyika kupitia vipindi **12** vya redio, kimoja cha runinga na vipeperushi na mabango **3,000.**

51. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa mfumo wa utambuzi na ufuatiliaji

mifugo kwa njia ya hereni kwa ng'ombe wa maziwa na ng'ombe wa nyama wafugwao kibiashara ambapo ng'ombe **100,000** na wafugaji **1,000** watatambuliwa. Aidha, utambuzi kwa kutumia chapa na usajili wa wafugaji utasisitizwa utekelezwe na Mamlaka zote za Serikali za Mitaa.

**Uwekezaji katika Sekta ya Mifugo**

52. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 Sekta binafsi imeendelea kutumia fursa ya mazingira mazuri ya uwekezaji ambapo wawekezaji wamewekeza katika ujenzi wa machinjio na viwanda vya kusindika nyama na kufanya idadi ya viwanda kuongezeka kutoka **15** mwaka 2013/2014 hadi **25** mwaka 2014/2015 (**Jedwali Na. 1**). Aidha, uwekezaji katika viwanda vya kusindika maziwa umeongezeka kutoka viwanda **74** mwaka 2013/2014 hadi **82** mwaka 2014/2015 vyenye wastani wa kusindika lita **490,000** kwa siku (**Jedwali Na. 7).** Vilevile, uwekezaji katika usindikaji wa zao la ngozi umeongezeka kutoka viwanda **7** mwaka 2013/2014 hadi tisa (**9**) mwaka 2014/2015 vyenye uwezo wa kusindika ngozi za ng'ombe vipande **4,634,000** na ngozi za mbuzi na kondoo vipande **22,820,000** kwa mwaka **(Jedwali Na. 8).**

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itahamasisha sekta binafsi kuwekeza katika usindikaji wa mazao ya mifugo kwa ajili ya kuongeza thamani, ajira, lishe na pato la Taifa kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo.

### 4.6 Uendelezaji wa Sekta ya Uvuvi

**Uvunaji wa Samaki na Uuzaji wa Mazao ya Uvuvi**

53. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa Sekta ya Uvuvi katika kukuza uchumi, uhakika wa chakula, kuongeza kipato, ajira na kupunguza umaskini, Wizara imeendelea kuhamasisha wavuvi na wadau wengine wa uvuvi kuhusu njia endelevu za uvunaji na matumizi ya rasilimali za uvuvi. Katika mwaka 2014/2015, Wizara ilitoa elimu kuhusu mfumo wa usimamizi wa rasilimali za uvuvi unaozingatia Ikolojia na Mazingira kwa Maafisa Uvuvi **21** na wakusanyaji wa takwimu za uvuvi **94** katika Jiji la Tanga, Manispaa za Kinondoni, Temeke, Ilala, Kigoma Ujiji, Sumbawanga na Halmashauri za Mkinga, Pangani, Bagamoyo, Kilwa, Mafia, Mkuranga, Kigoma, Uvinza, Mpanda, Nkasi na Kalambo. Vilevile, mafunzo kuhusu mfumo mpya wa uingizaji wa takwimu za mazao yanayosafirishwa nje ya nchi na yanayoingizwa nchini yalitolewa kwa Maafisa Uvuvi **6** kutoka

Ukanda wa Ziwa Victoria. Elimu hiyo imesaidia kuboresha ukusanyaji, uchakataji, usambazaji wa takwimu na matumizi sahihi ya zana bora za uvuvi.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara ilifanya sensa ya uvuvi katika Ukanda wa Ziwa Victoria, matokeo yanaonesha kuwepo kwa wavuvi **103,540**, zana za uvuvi **7,483,529**, vyombo vya uvuvi **29,154** na injini za kupachika **9,416.** Aidha, Ziwa lina jumla ya mialo **642** ya kupokelea samaki, kati ya mialo hiyo **25** imeboreshwa. Pia, Sensa ya Uvuvi ilifanyika katika maziwa madogo ya Tlawi, Manyara, Burunge, Basuto, Eyasi, Babati na Bwawa la Nyumba ya Mungu na matokeo yalionesha kuwepo kwa wavuvi **1,387,** vyombo vya Uvuvi **558**, zana za uvuvi **1,695** na mialo **20**.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** idadi ya wavuvi imeongezeka kutoka **183,431** mwaka 2013/2014 hadi wavuvi **183,800** mwaka 2014/2015 sawa na ongezeko la asilimia **0.25**. Aidha, vyombo vya Uvuvi vimepungua kwa asilimia **0.16** kutoka vyombo **57,385** mwaka 2013/2014 hadi vyombo vya uvuvi **57,291** mwaka 2014/2015. Jumla ya tani **369,827** za samaki zinazokadiriwa kuwa na thamani ya shilingi **trilioni 1.4** zilivunwa mwaka 2014/2015 ikilinganishwa na tani **367,854**

zenye thamani ya shilingi **trilioni 1.3** zilizovunwa mwaka 2013/2014 sawa na ongezeko la asilimia **0.53** (**Jedwali Na. 9a**).

56. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia biashara ya samaki na mazao ya uvuvi nje ya nchi kwa kuzingatia viwango vya kitaifa, kimataifa na mahitaji maalum ya masoko. Katika mwaka 2014/2015, tani **43,354** za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo **42,100** ziliuzwa nje ya nchi na kuiingizia Serikali mrabaha (*export royalty*) wa shilingi **bilioni 7.5** ikilinganishwa na tani **38,574** na samaki hai wa mapambo **44,260** zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2013/2014 na kuiingizia Serikali kiasi cha shilingi **bilioni 6.1** (**Jedwali Na. 9b**).

57. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia uvunaji na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi nchini. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha jamii za wavuvi kusimamia, kuendeleza na kutunza rasilimali za uvuvi kwa kuzingatia mfumo wa ikolojia na mazingira. Vilevile, Wizara itafanya sensa saba **(7)** za uvuvi na kufuatilia ukusanyaji, uchambuzi na utunzaji wa takwimu za uvuvi katika maeneo ya maji makubwa na madogo.

**Uwezeshaji Wavuvi na Wafugaji wa Samaki**

58. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta binafsi imeendelea kusambaza kwa wadau teknolojia na matumizi sahihi ya miundombinu kuhusu uandaaji, uchakataji, usambazaji na uuzaji wa mazao ya uvuvi yenye ubora na salama. Jumla ya wadau **374** wa uvuvi kutoka Mikoa ya Pwani, Bagamoyo (**37**), Mafia (**35**), Rufiji (**35**) Mkuranga (**32**) na Lindi katika wilaya ya Kilwa (**39**), Mwanza (**43**), Mara (**97**) na Rukwa (**56**) walinufaika na teknolojia na miundombinu hiyo ambayo imewawezesha kuongeza thamani na kukidhi mahitaji ya soko.

59. ***Mheshimiwa Spika***, kupitia ufadhili wa Programu ya SmartFish, Wizara iliwawezesha wachakataji saba (**7)** wa zao la dagaa kutoka mikoa ya Dar es Salaam (**3**), Mwanza (**3**) na Kagera (**1**) pamoja na Afisa Uvuvi (**1**) kushiriki maonesho ya kikanda ya mazao ya uvuvi yaliyofanyika Entebbe Uganda. Wadau hao walipata fursa ya kujifunza mbinu mbalimbali za uhifadhi na masoko ya mazao ya uvuvi.

60. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kushirikiana na Halmashauri mbalimbali katika kuboresha miundombinu na masoko ya mazao ya uvuvi. Katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika

jumla ya mialo minne (**4**) ya uvuvi ya Kibirizi (Kigoma-Ujiji), Muyobozi (Uvinza), Ikola (Mpanda) imekamilika na mwalo wa Kirando (Nkasi) ujenzi unakamilishwa. Aidha, Wizara imewezesha soko la samaki la Kasanga kwa kulipatia jenereta mbili za kuzalisha umeme na kuweka mfumo wa maji na umeme. Katika Ukanda wa Pwani, Wizara imekamilisha ujenzi wa vibanda vya kuhifadhi mitambo ya barafu katika Halmashauri za Mafia (Kilindoni), Kilwa (Masoko pwani) na Rufiji (Nyamisati).

61. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Benki ya Dunia imeandaa Mradi wa *Southwest Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth Programme (SWIOFish)* unaotarajia kuanza Julai, 2015. Mradi huu unalenga kuboresha fursa za kiuchumi, kijamii na mazingira miongoni mwa jamii za wavuvi kutokana na rasilimali za uvuvi katika Bahari ya Hindi.

62. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2014/2015 vikundi **51** kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa vimehakikiwa kwa ajili ya kupatiwa ruzuku kwa ajili ya zana na pembejeo za uvuvi. Aidha, ruzuku hiyo itatolewa kwa kufuata mwongozo ambapo wadau watachangia asilimia **60** na Serikali kuchangia asilimia **40**. Pia, wafugaji wa samaki watapata ruzuku ya chakula cha samaki kwa bei nafuu ya shilingi

**500/=** kwa kilo, sawa na punguzo la asilimia **84** ya bei halisi kupitia vituo vya Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi - FETA vilivyoko Mbegani – Bagamoyo, Nyegezi – Mwanza, Kibirizi – Kigoma na Mtwara.

63. ***Mheshimiwa Spika,*** katika juhudi za kuwawezesha wavuvi, Wizara kwa kushirikiana na mifuko ya Hifadhi ya Jamii inahamasisha wavuvi kujiunga na mifuko hii, ili kunufaika na mafao na huduma mbalimbali zinazotolewa na mifuko hiyo. Katika hatua za awali, Wizara na Mfuko wa Hifadhi ya Taifa wa Jamii – NSSF waliwekeana Makubaliano ya Utekelezaji ujulikanao kama "WAVUVI SCHEME" ambapo mpaka sasa Mfuko umesajili jumla ya wavuvi **1,234** katika Ukanda wa Ziwa Victoria. Lengo likiwa ni kusajili wavuvi **75,000** kwa Ukanda huo.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaanza utekelezaji wa Mradi wa *Southwest Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth Programme – SWIOFish*. Vilevile, Wizara itaendelea kuwawezesha wavuvi wadogo kupitia mfumo wa ruzuku na kuhamasisha wavuvi kujisajili na kujiunga katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya Taifa ili wafaidike na huduma zinazotolewa na mifuko hiyo. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu kuhusu fursa za uwekezaji na matumizi endelevu ya rasilimali za

uvuvi na kuhamasisha Sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya kutengeneza boti hususan za *fibre* na zana za uvuvi zinazokubalika kisheria. Vilevile, wadau **400** wa uvuvi watahamasishwa kuhusu uchakataji wa samaki na mazao yake na kuwezesha ujenzi wa chanja za kuanikia samaki katika mwambao wa Ukanda wa Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Bahari ya Hindi.

**Ukuzaji wa Viumbe kwenye Maji**

64. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, jumla ya vifaranga vya samaki **8,090,000** vimezalishwa na kusambazwa kwa wafugaji wa samaki. Kati ya hivyo, vifaranga **290,000** vimezalishwa katika vituo vya Serikali vya Kingolwira (Morogoro) **5,000**, Luhira (Songea) **200,000**, Mwamapuli (Igunga) **25,000** na Mtama (Lindi) **60,000**. Vilevile, vifaranga **7,800,000** vimezalishwa katika vituo binafsi vya Eden Agri Aqua Services (Dar es Salaam) **2,400,000**, Faith Aquaculture Services (Pwani) **1,800,000**, Olive Enterprises (Pwani) **1,200,000** na J & B Ruhanga Fish Culture Co. Ltd (Kagera) **2,400,000**. Pia, shamba la ufugaji wa kambamiti la Alphakrust (Mafia) lilizalisha vifaranga **11,000,000**. Aidha, wadau **3,582** wamehamasishwa na kupatiwa elimu ya ukuzaji viumbe kwenye maji. Kutokana na uhamasishaji huo, mabwawa yameongezeka kutoka **20,493**

mwaka 2013/2014 hadi **21,300** mwaka 2014/2015 ambapo uzalishaji wa samaki umeongezeka kutoka tani **3,000** hadi tani **3,118**.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kuimarisha Kituo cha Ukuzaji Viumbe kwenye Maji cha Mwamapuli (Igunga) kwa kujenga matangi **16** ya kutunza samaki wazazi na kukuzia vifaranga. Pia, miundombinu ya usambazaji maji na uzio wa kuimarisha usalama wa kituo vimejengwa. Aidha, kitotolishi (hatchery) chenye uwezo wa kuzalisha vifaranga **11,520,000** kwa mwaka kimeimarishwa kwa kuwekewa vifaa vya kutotoleshea vifaranga vya samaki. Vilevile, kituo cha Kingolwira kimeimarishwa kwa kujenga kitotolishi, kuchimba kisima kirefu na kukarabati mabwawa manne **(4)** na matangi **21** ya kuzalishia vifaranga. Pia, kituo cha Luhira kimeimarishwa kwa kukarabati bwawa lenye ukubwa wa mita za mraba **14,600** na kupandikizwa samaki **56,000**. Vilevile, kituo cha Nyengedi (Lindi) kimeanzishwa kwa kuchimba mabwawa manne (**4**), mtaro wa kuingiza maji kwenye mabwawa pamoja na kujenga jengo kwa ajili ya ofisi.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Kituo cha Machui kimeimarishwa kwa kujengwa bwawa moja **(1)** lenye ukubwa wa

mita za mraba **1,200** na kupandikiza samaki wazazi **1,000**. Aidha, ukaguzi wa usalama na ubora katika mashamba ya ukuzaji viumbe kwenye maji umefanyika ambapo imebainika kuwa, sampuli zilizowasilishwa zipo katika viwango vinavyokubalika. Uzalishaji wa Kambamiti wa kufuga umeongezeka kutoka tani **320** zenye thamani ya shilingi **bilioni 2.56** mwaka 2013/2014 hadi tani **391** zenye thamani ya shilingi bilioni **3.2** mwaka 2014/2015 .Aidha, uvunaji wa Mwani umeongezeka kutoka tani **179.3** zenye thamani ya shilingi **84,370,000** mwaka 2013/2014 hadi tani **222.8** mwaka 2014/2015 zenye thamani ya Shilingi **133,200,000.**

67. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuboresha ukuzaji wa viumbe kwenye maji kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuimarisha vituo **11** vya ufugaji wa samaki wa maji baridi kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa vifaranga **milioni 10** mwaka 2015/2016;

(ii) Kuendeleza vituo viwili (**2**) vya Mbegani na Machui vya ufugaji wa samaki wa maji bahari kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa vifaranga **milioni 3** mwaka 2015/2016;

(iii) Kuandaa miongozo kwa ajili ya matumizi ya teknolojia mpya zinazoibuka pamoja na kuanisha samaki wengine wenye sifa za kufugwa;

(iv) Kufanya ufuatiliaji kwa ajili ya kuzuia na kudhibiti magonjwa ya viumbe wakuzwao kwenye maji ili kuongeza thamani ya mazao; na

(v) Kuanzisha kituo cha ukuzaji viumbe kwenye maji bahari Mtwara.

### 4.7 Utafiti, Mafunzo na Ugani wa Mifugo na Uvuvi

68. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara imeimarisha miundombinu ya utafiti wa mifugo na uvuvi kwa kuiwezesha TALIRI kununua mashine mbili (**2**) za kukatia nyasi kwa ajili ya mifugo, jembe la trekta (**1**) pamoja na Tela moja (**1**) na kukamilisha uwekaji wa miundombinu ya kusambaza umeme katika kituo cha West Kilimanjaro. Pia, TAFIRI imewezeshwa kununua magari mawili **(2)** aina ya “pick-up double cabin” na boti tano **(5)** aina ya “fibre glass” zenye injini za uwezo wa “Horse Power (HP)” **15** kila moja. Boti hizi zitaiwezesha TAFIRI kufanya tafiti mbalimbali katika kina kifupi cha mito, maziwa na bahari.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakiki na kuratibu program za utafiti zinazoendana na vipaumbele vya Taifa, katika mwaka 2014/2015, Wizara imekamilisha uandaaji wa Ajenda ya Kitaifa ya Utafiti wa Mifugo (Livestock Research Agenda) ambapo jumla ya nakala **500** zilichapishwa na kusambazwa kwa wadau. Aidha, Wizara imekamilisha uandaaji wa Ajenda ya Kitaifa ya Utafiti wa Uvuvi ambayo iko katika hatua ya uchapishaji.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara iliandaa mikakati ya kutathmini, kuibua miradi mipya na kuboresha kiwango cha upatikanaji na usambazaji wa matokeo ya tafiti za mifugo na uvuvi kwa wadau. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na FAO na USAID ilifanya utafiti wa kuangalia mbari za mbuzi wa asili ambapo jumla ya sampuli **131** kutoka Wilaya za Arumeru, Babati, Mvomero, Ngorongoro na Siha zilikusanywa na kupelekwa maabara za Idara ya Kilimo ya Marekani (USDA) kwa uchunguzi zaidi.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara iliendelea kujenga uwezo kwa watafiti ili kuongeza ufanisi wa utafiti unaokubalika Kimataifa, ambapo watafiti **37** walipatiwa mafunzo ya kuibua na kuandika tungo za utafiti na machapisho. Aidha, mfumo wa ukusanyaji, utunzaji na usambazaji wa

taarifa za matokeo ya utafiti wa mifugo nchini uliandaliwa ambapo jumla ya nakala **4,000** za vijitabu vya Ufugaji Bora wa Mbuzi wa Maziwa, Ufugaji Bora wa Nguruwe na Ukulima wa Malisho vimeandaliwa, kati ya hivyo vijitabu **2,000** vimesambazwa kwa wadau.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na mabadiliko ya teknolojia mpya zinazohitajika katika kuzalisha na kutunza mifugo, katika mwaka 2014/2015, Wizara imeandaa na kutekeleza Mpango wa Kurithisha Majukumu kwa wataalam wa utafiti. Aidha, watafiti **31** wanapatiwa mafunzo katika ngazi za shahada za uzamili **(26)** na uzamivu **(5)** ndani ya nchi. Katika kipindi hicho, jumla ya watumishi watano (**5)** wameajiriwa.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuratibu na kutathmini utafiti na huduma za utafiti na maendeleo ya ufugaji na uvuvi kulingana na program zake. Aidha, Wizara kwa kupitia Taasisi za utafiti na Wakala zake itaendelea kutathmini maeneo ya utafiti, kuibua miradi mipya na kuboresha kiwango cha upatikanaji na usambazaji wa matokeo ya tafiti za mifugo na uvuvi kwa wadau. Vilevile, Wizara itaendelea kuratibu tafiti za mifugo pamoja na kuimarisha ushirikiano na mataifa mengine katika masuala ya utafiti.

**Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI)**

74. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) kwa kuboresha miundombinu, kuipatia vitendea kazi ikiwa ni pamoja na kununua tela (**1**) la trekta, jembe (**1**) la trekta, na mashine (**2**) za kukatia malisho yaani (*Mower*) kwa ajili ya vituo vya Mpwapwa, Kongwa, Uyole na West Kilimanjaro na kupatiwa rasilimali watu. Aidha, Taasisi imekamilisha Muundo wa Utumishi na Mkakati wa Kibiashara na inaendelea kupitia Kanuni za Fedha na Kanuni za Utumishi ili kuboresha utendaji wake kwa mujibu wa Sheria Na. 4 ya mwaka 2012 iliyounda TALIRI.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, TALIRI imeendelea kutekeleza jumla ya miradi **59** ya utafiti kupitia vituo vyake saba **(7)** vya Mpwapwa, Tanga, Uyole, West Kilimanjaro, Kongwa, Mabuki na Naliendele. Kati ya miradi hiyo, **15** ni utafiti wa tasnia ya maziwa, **12** ni tasnia ya nyama, **6** ni utafiti wa mbuzi na kondoo, **15** ni uendelezaji wa malisho na **11** kuku na nguruwe. Aidha, TALIRI kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) imezalisha ng’ombe **6** aina ya

*Bonsmara* kwa kutumia Tekonolojia ya Uhawilishaji wa Viini Tete (MOET). Majaribio haya ya awali ya Uhawilishaji yamedhihirisha kuwa mbari za mifugo bora zinaweza kupatikana kwa njia hii pia na kwa kuhusisha mifugo iliyopo katika mazingira ya nchi yetu.

**Usambazaji wa mifugo bora**

76. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, TALIRI imesambaza jumla ya ng'ombe **131** aina ya Mpwapwa yakiwemo madume **51** na majike **80.** Ng'ombe hao walisambazwa katika maeneo ya Chamwino (madume **4,** jike **1**), Dar es Salaam (Madume **13**, majike **12**), Dodoma (Madume **10**, Majike **4**), Kibaha (Madume **3**, Majike **4**), Kongwa (Madume **11**, majike **5**), Nyamagana (Majike **2**), Mpwapwa (madume **10**, majike **15**), Manyoni (dume **1**), Musoma (majike **2**, madume **10**) na Ngorongoro (madume **4**, majike **18**) kwa ajili ya kuzalisha mifugo bora na kuboresha ng'ombe wa asili. Aidha, taasisi imeendelea kutunza ng'ombe **1,987,** katika vituo vyake kwa ajili ya utafiti kwa lengo la kuzalisha na kusambaza matokeo ya tafiti. Vile vile, madume **4** yalipelekwa NAIC-Arusha kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora za uhimilishaji. Pia, jumla ya ng'ombe bora **26** (madume **24**, majike **2**) wa maziwa aina ya *Friesian* walisambazwa katika Halmashauri za Rungwe (madume **8**, majike **2**), Mbozi (madume

**4**), Jiji la Mbeya (madume **6**); Mbeya (madume **3**) na Mufindi (madume **3**).

77. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 jumla ya mbuzi bora **114** walisambazwa kwa wafugaji kwa ajili ya kuongeza uzalishaji katika maeneo ya Kibaha (**36**); Kongwa (**34**); Dar es Salaam (**2**); Tanga (**2**); Newala (**14**);Bahi (**10**); Dodoma (**4**); Chamwino (**2**); Kinondoni (**8**) na Mpwapwa (**2**). Vilevile, jumla ya nguruwe **127** kutoka katika kituo cha TALIRI-Mpwapwa walioboreshwa (madume **45** na majike **82**) walisambazwa kwa wafugaji katika maeneo ya Mpwapwa (madume **11,** Majike **25**), Kongwa (Madume **5,** Majike **25**) na Chamwino (madume **29**, majike **32**). Aidha, jumla nguruwe **140** walioboreshwa kutoka katika kituo cha TALIRI-Uyole (madume **61,** majike **79**) walisambazwa katika Halmashauri za Makete (madume **2**, majike **9**); Jiji la Mbeya (madume **6**, majike **6**); Mbeya (madume **4**, majike **2**); Njombe Mji (madume **20**, majike **24**); Njombe (madume **3**, majike **4**); Wanging'ombe (madume **5**, majike **4**); Mbozi (madume **5**, majike **3**) na Rungwe (madume **17**, majike **26**).

78. ***Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za kubuni na kusambaza teknolojia za uzalishaji wa kuku wa asili, Taasisi imeendelea kutunza na kuhifadhi kosaafu za kuku wa asili ili kutathimini uwezo wao wa ukuaji na uzalishaji,

ambapo jumla ya kuku wa asili **650** waliendelea kutunzwa katika vituo vya TALIRI- Mpwapwa, Uyole, Naliendele na Tanga. Aidha, Utafiti umeonyesha kuwa kuku aina ya Horasi, Kishingo na Kuchi wana uwezo wa kutaga mayai **12-14** kwa mtago; kuku aina ya Katewa **18-20**; kuku aina ya Mandendega **16-17** na kuku aina ya Logashi na Sasamala (Frizzled) mayai **10-12** kwa mtago.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, TALIRI iliendesha mafunzo ya ufugaji bora ambapo wafugaji wa nguruwe **150** kutoka Halmashauri za Njombe na Rungwe walipata mafunzo ya ulishaji wa nguruwe ili kuongeza tija ya uzalishaji. Matokeo ya tathmini yameonyesha kuwa asilimia **53** ya wafugaji wa nguruwe katika Halmashauri za Njombe na Rungwe wamepokea teknolojia za ufugaji bora wa nguruwe. Aidha, jumla ya wafugaji wa nguruwe **35** kutoka katika Halmashauri za Njombe (**19**) na Rungwe (**16**) walipata sifa za kupewa madume bora ya nguruwe katika awamu ya pili ya usambazaji iliyotekelezwa katika miezi ya Novemba na Desemba, 2014. Vilevile, Wafugaji **50** kutoka Halmashauri za Magu, Mpwapwa na Misungwi walipata mafunzo ya njia bora za uboreshaji na uhifadhi wa malisho ya Mifugo. Pia, wafugaji **117** kutoka Halmashauri za Bagamoyo **(55)** na Muheza **(62)** walipata mafunzo juu ya kuongeza thamani ya

maziwa na njia bora ya ulishaji ng'ombe wa maziwa. Vilevile, kituo cha Mdaula cha kusindika maziwa kiliboreshwa ambapo miundombinu ya kusindika maziwa imejengwa.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na uhaba wa watumishi, watumishi wapya **13** wameajiriwa wakiwemo watafiti (**6**), maafisa ugavi (**2**), watunza kumbukumbu watatu (**3**), fundi sanifu wa maabara (**1**) na mhasibu (**1**). Aidha, jumla ya watafiti saba (**7**) wamepata shahada za uzamili katika nyanja za taaluma mbalimbali za utafiti wa mifugo. Pia, watafiti **17** wanaendelea na masomo ya shahada za uzamivu (**9**) na uzamili (**7**) na shahada ya kwanza (**1**). Vilevile, Wanafunzi wawili **(2)** wa shahada ya uzamili wanaendelea na masomo yao chini ya ufadhili wa EAAPP.

**Utafiti wa malisho ya Mifugo**

81. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 TALIRI iliendelea na tafiti zenye lengo la kujumuisha malisho bora katika mifumo ya uzalishaji na ikolojia mbalimbali na ilihusisha jumla ya wafugaji **264** kutoka Halmashauri za Misungwi, Magu, Kilwa na Lushoto. Aidha, Taasisi iliendelea kuhifadhi na kufuatilia ubora wa vinasaba **83** vya malisho katika benki zake za vinasaba za TALIRI Tanga, Uyole, Mpwapwa na Mabuki.

Katika kipindi hicho**,** marobota **67,329** ya malisho ya mifugo yalivunwa katika vituo vya Mpwapwa (**33,465**); Uyole (**9,000**); Kongwa (**1,500)**; Tanga (**20,000);** Mabuki (**600)** na West Kilimanjaro (**2,764)**. Aidha, kilogramu **35,000** za vishina vya malisho na kilogramu **3,160** za mbegu za malisho aina ya nyasi zimesambazwa kwa wafugaji.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI) na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela (NM-AIST) inatekeleza mradi wa miaka miwili (2) kuanzia 2015-2017 wenye lengo la kuongeza ufanisi katika uzalishaji na tija ya ng'ombe wa maziwa. Pia, Taasisi kwa kushirikiana na SUA na ILRI imekamilisha andiko la Mradi wa uboreshaji wa kuku wa asili unaoanza kutekelezwa katika Nchi za Tanzania, Ethiopia na Nigeria. Miradi hii inafadhiliwa na Taasisi ya *Bill and Melinda Gates Foundation*. Vilevile, TALIRI kwa kushirikiana na watafiti kutoka nchi za Msumbuji na Zambia wanatekeleza miradi yenye lengo la kuongeza tija katika uzalishaji wa kuku wa asili na mradi wa ukusanyaji na usindikaji wa maziwa ili kuongeza kipato na uhakika wa chakula. Miradi hii inafadhiliwa na Umoja wa Nchi za Ulaya (EU) kupitia Kituo cha Kimataifa cha Kuratibu Utafiti

wa Kilimo Kusini mwa Afrika (*Center for Coordination of Agricultural Research and Development in Southern Africa* (CCARDESA)).

83. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuimarisha utafiti wa mifugo kwa kuboresha miundombinu ya mashamba ya vituo vya TALIRI, kuvipatia vitendea kazi pamoja na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi. Aidha, kwa kushirikiana na wadau wa utafiti wa ndani na nje ya nchi, TALIRI itaendelea kutekeleza miradi ya utafiti wa mifugo na malisho kwa lengo la kuongeza tija katika uzalishaji wa nyama, maziwa, mayai na mazao mengine ya mifugo ili kuboresha lishe, kipato na usalama wa chakula.

**Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI)**

84. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi kwa lengo la kundeleza sekta ya Uvuvi. Taasisi imeendelea kufanya utafiti na kuishauri Serikali na wadau wa uvuvi kuhusu hali ya rasilimali za uvuvi na jinsi ya kuzihifadhi na kuzivuna kwa uendelevu. Ushauri huo umetolewa kupitia tafiti mbalimbali, ikiwemo tathmini ya uwingi wa samaki aina ya sangara (Hydro-acoustic survey) katika Ziwa Victoria ambapo matokeo yanaonesha kiasi cha Sangara Ziwa Victoria

kuongezeka kwa kipimo cha uwingi (biomass) kutoka tani **939,724** mwaka 2011 mpaka tani **1,230,436** mwaka 2014 kutokana na kuimarika kwa udhibiti wa matumizi ya rasilimali za uvuvi. Aidha, uwingi wa dagaa umeongezeka na wa jamii za furu umeshuka kutokana na ongezeko la sangara ambao chakula chao ni furu.

85. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kulinda mazalia ya samaki, TAFIRI kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kupitia ufadhili wa LVEMP II inatekeleza mradi wa uhifadhi wa Ghuba ya Nyegezi ili kuboresha Bioanuwai ya eneo hilo na Ziwa Victoria kwa ujumla. Aidha, tathmini ya athari kwenye Mazingira (EIA) na Uchumi-Jamii katika mradi huu ilifanyika na kuonesha kwamba eneo hilo ni mojawapo ya mazalia ya samaki na hivyo linafaa kuhifadhiwa kama eneo tengefu kwa ajili ya mazalia na makulia ya samaki na pia kwa utalii wa mazingira na utafiti.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** Utafiti kuangalia mavuno ya samaki (catch assessment) na madhara ya minyoo (*Ligula intestinalis*) kwa Dagaa katika Ziwa Nyasa unaendelea. Utafiti huu utasaidia kujua kiasi cha samaki kinachopatikana kwa wavuvi na kuanisha madhara ya minyoo katika Dagaa. Tafiti hizi zitasaidia kuimarisha mpango wa kutunza rasilimali za Ziwa Nyasa kwa uvuvi endelevu.

Vilevile, Utafiti kuangalia jiolojia na sedimentolojia pamoja na ufuatiliaji wa unadhifu na ubora wa maji (Monitoring of the water quality) ya Ziwa Tanganyika unaendelea. Utafiti huu utasaidia kuelewa hali ya ziwa hivyo kuwezesha utunzaji wa bioanuwai ipatikanayo katika ziwa hilo kwa uvuvi endelevu. Pia, Utafiti uliofanyika katika Bwawa la Nyumba ya Mungu (BNM) kwa kushirikiana na watafiti toka Chuo Kikuu cha Bern, Switzerland umeonesha kuwa Sato (Nile tilapia) ambao hawakuwepo katika BNM kwa sasa wanapatikana kwa wingi. Kutokana na matatizo ya kiikolojia yaliyopatikana baada ya Sato kupandikizwa Ziwa Victoria ambapo Perege aina ya *Oreochromis esculenta* walipotea, hali hii inaleta shaka kwa *O. esculenta* wa BNM. Wizara kwa kushirikiana na TAFIRI itaendelea kufuatilia hali ya Sato na Perege katika BNM ili kuweza kutunza aina zote za samaki kwa manufaa ya wavuvi wa bwawa hilo.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** Utafiti mwingine uliofanyika katika Ziwa Masoko ambalo ni Ziwa la Kreta (Rungwe) umeonesha kuwa ziwa hili lina bioanuwai kubwa ya samaki. Aidha, sampuli za samaki aina ya Furu na Sato zimepelekwa Uingereza kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa vinasaba. Tafiti hii itasaidia kujua bioanuwai ya samaki katika maziwa ya Kreta yaliyo katika Bonde la Ziwa Nyasa. Maziwa haya

ni muhimu katika kutunza vinasaba vya samaki (Gene Bank), utalii wa kiikolojia (eco-tourism) na utafiti.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** TAFIRI imeendelea kufanya tafiti kwa kushirikiana na wafugaji wa samaki wa Mikoa ya Morogoro, Mwanza, Mara, Kagera, Arusha, Iringa, Ruvuma, Mbeya na Dar es Salaam ili kuboresha ufugaji wao uwe wa tija. Tafiti hizo zililenga utengenezaji wa vyakula bora vya samaki kwa kutumia malighafi zipatikanazo karibu na wafugaji, uzalishaji mbegu (vifaranga) bora vya samaki na ufugaji wa mfumo wa mseto unaojumuisha samaki, kilimo cha mbogamboga na kuku. Vilevile, TAFIRI imeendelea na uzalishaji wa mbegu bora za samaki kwa kushirikisha wafugaji wa samaki. Uzalishaji huu umefanyika katika eneo la Mwakalima (Misungwi) na vifaranga **7,000** vya kambale vimezalishwa na kusambazwa. Aidha, Taasisi kwa kushirikiana na wafugaji wa samaki wa Nyasoro (Rorya) inaendelea na ujenzi wa kitotoleshi cha kuzalishia vifaranga vya Kambale ili kuwasaidia wafugaji kuongeza kipato kwa kuuza vifaranga.

89. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Taasisi pia imeendelea na ukusanyaji wa Takwimu za uvuvi wa pweza katika mialo ya Tanga, Mtwara na Pwani kwa lengo la kupata hali halisi ya nguvu ya uvuvi wa

Pweza, aina ya Pweza wapatikanao na Biolojia yao. Takwimu hizi zitasaidia kuimarisha mpango wa kuwatunza kwa uvuvi endelevu. Pia takwimu zitasaidia katika "certification" ya Pweza wapatikanao Tanzania ili kuimarisha soko lao na kukuza uchumi wa Taifa. Aidha, majaribio ya ukaushaji dagaa kwa kushirikiana na wavuvi wa dagaa katika Ziwa Nyasa yanaendelea, ambapo tathimini ya kimaabara ya viinilishe vya dagaa waliokaushwa kwa jua kutumia jiko la *solar*, vichanja na ardhini imefanyika. Matokeo ya awali yanaonesha kuwa viinilishe katika dagaa waliokaushwa kwa jiko la *solar* ni bora kuliko aina nyingine ya ukaushaji. Matokeo ya utafiti huu yatasaidia jamii za wavuvi walio katika Ziwa Nyasa kupunguza uharibifu wa samaki baada ya mavuno ambalo ni tatizo kubwa linaloshusha mapato ya wavuvi.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Taasisi imetoa matokeo ya tafiti zake kwa Serikali na wadau wa uvuvi kupitia makongamano, mikutano, warsha, vyombo vya habari kama vile luninga, magazeti, vipeperushi, machapisho katika majarida ya kisayansi, na sikukuu za kitaifa kama Mei Mosi, Nane Nane, Siku ya Mvuvi Duniani na Wiki ya Utumishi.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imewawezesha jumla ya wafanyakazi **27** kuendelea na mafunzo katika ngazi ya shahada ya uzamivu **18**, uzamili

**8** na ya kwanza **1** kwa ufadhili wa Serikali kupitia COSTECH na wafadhili wa nje. Katika kipindi hicho, wafanyakazi **7** walihitimu mafunzo ya shahada za uzamivu mmoja (**1**), uzamili wanne (**4**) na ya kwanza wawili (**2**). Vilevile, katika kipindi tajwa wafanyakazi **15** walihudhuria mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali nchini na nje ya nchi. Taasisi imewezeshwa kununua magari mawili (**2)** aina ya "Toyota pick-up double cabin" na boti tano (**5**) aina ya "fibre" zenye injini za uwezo wa nguvu za farasi **15** kila moja kwa vituo vyake vinne (**4**) vya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma na Kyela, pamoja na kituo kidogo cha Sota, Rorya. Boti hizi zitaiwezesha TAFIRI kufanya tafiti mbalimbali katika kina kifupi cha mito, maziwa na bahari. Pia, boti moja aina ya "rubber dingy" na vifaa vya uzamiaji vimenunuliwa kwa ajili ya kituo cha Kyela.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016 TAFIRI kwa kushirikiana na wadau wengine wa uvuvi itaendelea na tafiti za samaki na mazingira katika maziwa makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa), maziwa ya kati (Rukwa, Kitangiri na Eyasi), maziwa madogo, mito na Bahari ya Hindi; kufanya utafiti wa ufugaji samaki hasa katika maeneo yaliyo na changamoto kama vile upatikanaji wa mbegu bora, vyakula bora vya samaki na teknolojia bora ya ufugaji katika maeneo tofauti; kufanya

utafiti wa kupunguza uharibifu wa mazao ya samaki baada ya uvunaji; kuimarisha miundombinu ya Taasisi kwa kujenga ofisi na maabara ya kituo cha Dar es Salaam na Sota, kukarabati na kununua vitendea kazi vya kitafiti pamoja na vifaa vya maabara kwa vituo vyake vinne vya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma na Kyela, pamoja na kituo kituo kidogo cha Sota (Rorya) na Makao Makuu. Aidha Taasisi itaendelea kusambaza taarifa za kitafiti kwa wadau mbalimbali wa uvuvi.

**Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (Tanzania Veterinary Laboratory Agency-TVLA)**

93. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) umeendelea kufanya utambuzi na uchunguzi wa magonjwa kwenye sampuli za mifugo, wanyamapori na ndegepori kupitia maabara zake za Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Tabora, Dodoma, Iringa na Mtwara. Katika mwaka 2014/2015 TVLA imepokea katika maabara zake jumla ya sampuli **6,909** kwa ajili ya ufuatiliaji wa mienendo ya magonjwa ya wanyama hapa nchini. Magonjwa yaliyotambuliwa ni pamoja na;- kwa ngómbe-Ugonjwa wa Kutupa Mimba **(353),** Ndigana Kali **(31),** Ndigana Baridi **(45),** Minyoo **(16),** Kimeta **(8);** Sotoka ya Mbuzi na Kondoo **(99),** Homa ya

Mapafu ya Mbuzi **(10);** Kichaa cha Mbwa **(22);** Kuku- Minyoo **(529),** Mdondo **(332),** Gumboro **(73),** Kuhara **(320)** na Kuhara Damu **(669);** na Ndege Pori- Mdondo **(30).**

94. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya uzalishaji wa chanjo (TVI) Kibaha imeendelea kuzalisha chanjo dhidi ya ugonjwa wa mdondo wa kuku ambao bado unaongoza kwa kuua kuku wengi wa asili katika sehemu nyingi za nchi yetu. Katika mwaka 2014/2015 jumla ya dozi **24,500,000** za chanjo ya mdondo zimezalishwa na kusambazwa kwa wafugaji wa kuku katika Halmashauri zote hapa nchini. Chanjo hii imeonesha mafanikio makubwa ya kuzuia vifo kwa asilimia **95** kwa wafugaji wanaotumia chanjo hii katika mikoa ambayo imekuwa ikichanja kuku kwa kampeni hususan mikoa ya Singida, Iringa, Njombe, Mbeya na Ruvuma.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** Maabara kuu ya Mifugo, Temeke imeendelea kufanya uhakiki wa ubora wa vyakula vya mifugo vinavyozalishwa na kutumiwa na wafugaji hapa nchini. Katika mwaka 2014/2015 jumla ya sampuli **1,644** za vyakula vya mifugo kutoka katika makampuni na wafugaji zilifanyiwa uhakiki. Katika uhakiki huo, asilimia **92** ya vyakula hivyo vilikuwa na viwango vya ubora unaotakiwa na sampuli chache zilionekana kuwa na upungufu wa protini, nguvu, wanga na unyevu mwingi. Aidha,

Watengenezaji wa vyakula walishauriwa kuzingatia kanuni za uzalishaji wa vyakula bora vya mifugo.

96. ***Mheshimiwa Spika,*** TVLA imeendelea kukamilisha vigezo vya kupata ithibati ya kimataifa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya umahiri wa maabara (ISO 17025). Katika kutekeleza hilo, Wakala umewezesha mafunzo ya ndani kwa watumishi wa maabara, umekarabati maabara na kununua vifaa na vitendanishi vinavyotumika kwenye teknolojia za uchunguzi wa magonjwa na uhakiki wa ubora wa vyakula vya mifugo zinazokusudiwa kupatiwa ithibati. Aidha, mtaalamu mwelekezi amefanya tathmini ya awali ya ukamilishaji wa vigezo katika maabara kuu ya mifugo, Temeke na taarifa inaonesha kuwa Wakala umekidhi vigezo vingi vinavyohitajika.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, TVLA itaendelea kufanya kazi ya utambuzi, uchunguzi na utafiti wa magonjwa ya mifugo na kuimarisha vituo vyake kwa kuvikarabati na kuvipatia vitendea kazi. Aidha, itaendelea kuzalisha na kusambaza dozi **milioni 100** za chanjo ya Mdondo, dozi **500,000** za chanjo ya Kimeta na dozi **500,000** za chanjo ya Chambavu. Pia, itaweka mikakati ya kuzalisha zaidi chanjo ya mdondo na kuuza katika nchi jirani ili kuongeza mapato. Vilevile, itaendelea

kufanya uhakiki wa vyakula vya mifugo vinavyozalishwa na kutoa ushauri stahiki kwa wazalishaji na wafugaji na itakamilisha taratibu za kupata ithibati ya ISO 17025.

**Mafunzo katika Vyuo vya Mifugo na Uvuvi**

**Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (Fisheries Education and Training Agency - FETA)**

98. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) kutoa mafunzo ya wataalam katika sekta ya uvuvi ambapo udahili wa wanachuo wa Kozi za astashahada na stashahada umeongezeka kutoka **1,073** mwaka 2013/2014 hadi kufikia **1,180** kwa mwaka 2014/2015. Aidha, Wakala umeendesha mafunzo ya Kozi fupi kwa maafisa ugani na wavuvi wapatao **1,390** nchini, ikiwa ni pamoja na wavuvi **100** kutoka Tanzania bara **(50)** na Zanzibar **(50)** waliopatiwa mafunzo maalumu ya mbinu za kuvua katika bahari kuu (*Deep Sea Fishing*). Vilevile, FETA imetoa mafunzo ya kozi za uvuvi kwa maafisa uvuvi **122** kutoka nchi za Uganda, Kenya, Burundi, Rwanda na Somalia.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia FETA imeendelea kuongeza udahili wa wanafunzi kwa kuimarisha miundombinu na

kupanua Kampasi za FETA za Mbegani (Bagamoyo), Nyegezi (Mwanza), Kibirizi (Kigoma), Mikindani (Mtwara) na Gabimori (Rorya). Aidha, madarasa **(4)** yamejengwa katika vituo vya Mwanza South (Mwanza) **(2)** na Mikindani (Mtwara) **(2)**. Vilevile, wakufunzi **10** wamehitimu masomo ya Shahada za Uzamili na **12** wanaendelea na masomo ya shahada ya uzamili na mmoja **(1)** ameanza masomo ya Shahada ya Uzamivu nchini Ujerumani. Katika kipindi hiki watumishi **15** wameajiriwa wakiwemo wakufunzi nane **(8).**

100. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuiwezesha FETA kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuongeza udahili wa wanafunzi wa astashahada na stashahada kutoka **1,180** hadi **1,500;** kukamilisha ujenzi wa vituo vya Gabimori na Mtwara Mikindani na kukarabati Kampasi za Nyegezi, Mbegani na Kigoma. Aidha, kituo kipya cha Mbamba Bay kitaanzishwa.

**Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (Livestock Training Agency - LITA)**

101. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara imewezesha Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA) kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka **2,215** hadi **2,451** (Stashahada **988** na Astashahada **1,463**). Kati

ya hao, **1,612** watamaliza mafunzo yao mwezi Juni 2015 wakiwemo **737** wa Stashahada na **875** wa Astashahada. Aidha, watumishi **42** wanaendelea na mafunzo katika ngazi ya Shahada za Uzamivu watatu **(3),** Uzamili **16,** ya Kwanza **19** na Stashahada wanne **(4).** Pia, Wizara imekamilisha Mwongozo wa Kutoa Mafunzo ya Mifugo (*Livestock Training* Guidelines) kwa ajili ya vyuo vyote nchini.

102. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha vyuo vya mifugo ambapo hadi sasa jumla ya vyuo vya mafunzo ya mifugo **21** vinavyotoa mafunzo katika ngazi ya astashahada na stashahada vimeanzishwa. Kati ya hivyo, vyuo vitano **(5)** vimetambuliwa na Bazara la Veterinari Tanzania na **16** vipo katika hatua ya kusajiliwa ambapo vyote vimepata ithibati ya NACTE. Vyuo hivyo vimedahili jumla ya wanafunzi **534** wa stashahada na astashahada**.** Aidha, Wakala umejenga madarasa matatu (**3**) katika Kampasi za Temeke, Mabuki na Kikulula, kukarabati mabweni manne (**4**) katika kampasi ya Tengeru na Buhuri na kununua vitendea kazi vikiwemo madawati **30,** kompyuta saba (**7)** na *solar panel* **24.**

Aidha, LITA imeendesha mafunzo ya muda mfupi kwa wafugaji na wadau wengine kuhusu afya na uzalishaji wa mifugo, ufugaji bora wa

ng'ombe wa maziwa, usindikaji wa maziwa, ufugaji bora wa nguruwe na kuku wa asili.

103. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuiwezesha Wakala kutekeleza majukumu yake na kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka **2,451** kufikia **2,500**. Aidha, wakala itahuisha na kuboresha mitaala ya muda mrefu na mfupi, kuandika vitabu vya kiada na rejea kwa mafunzo ya afya na uzalishaji wa mifugo na kutoa mafunzo ya mbinu za utafiti na kuandika miradi kwa wakufunzi **12**. Vilevile, wakala itatoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi na kuwezesha mafunzo ya ufugaji kibiashara kwa vijana ili waweze kujiajiri na itaandaa sera ya udhibiti wa majanga.

**Huduma za Ugani za Mifugo na Uvuvi**

104. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara iliandaa, kuratibu na kushiriki katika maonesho mbalimbali ya kitaifa kwa lengo la kuongeza elimu kwa wafugaji na wavuvi. Aidha, jumla ya wadau **862** walipatiwa elimu juu ya ufugaji bora wa ng'ombe, uvuvi endelevu na ufugaji bora wa samaki kupitia maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nanenane yaliyofanyika kitaifa mkoani Lindi. Vilevile, maadhimisho ya Siku ya Mvuvi Duniani yalifanyika Mkoani Kagera ambapo jumla ya

wadau **1,428** walipatiwa elimu ya uvuvi endelevu na ufugaji bora wa samaki.

105. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Bodi za Nyama na Maziwa imeendelea kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma za ugani kwa wafugaji, wavuvi na wakuzaji viumbe kwenye maji kwa lengo la kuongeza lishe, kipato na ajira kwa vijana. Huduma hizi zimetolewa kwa kuzingatia viwango vya ubora wa mazao ya mifugo na uvuvi kulingana na mahitaji ya soko.

106. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeongeza idadi ya wagani wa mifugo kutoka **6,041** mwaka 2013/2014 hadi **8,541** mwaka 2014/2015 kati ya **17,325** wanaohitajika. Idadi ya wagani wa uvuvi imeongezeka kutoka **510** mwaka 2013/2014 hadi **664** mwaka 2014/2015 kati ya **16,000** wanaohitajika. Aidha, jumla ya wafugaji **9,016** na wavuvi **6,800** wamepata elimu juu ya ufugaji wa kisasa na uvuvi endelevu. Pia, maafisa ugani wa mifugo **150** na uvuvi **47** walipatiwa mafunzo kuhusu mbinu bora za utoaji huduma za ugani. Vilevile, wafugaji **15** wa ng'ombe wa maziwa kupitia Mradi wa EAAPP walipata ziara ya mafunzo Naivasha, Kenya.

107. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa na Wizara ni pamoja na kuandaa

na kurusha hewani vipindi **28** vya redio na **48** vya luninga juu ya ufugaji, ukuzaji viumbe kwenye maji na uvuvi endelevu. Aidha, jumla ya nakala **14,500** za vijitabu viliandaliwa na kusambazwa kwa wadau, kati ya vijitabu hivyo nakala **1,000** ni za Mwongozo wa Huduma za Ugani, **2,000** ni za Kanuni za Ufugaji Bora na **11,500** ni za Ufugaji Bora wa Ng'ombe wa Maziwa na Ufugaji Bora wa Kuku wa Asili.

108. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara iliendelea kuboresha uzalishaji wa ng'ombe wa asili ili kuongeza uzalishaji wa maziwa ambapo kupitia mradi wa EAAPP, jumla ya madume bora **57** yalinunuliwa na kusambazwa katika vijiji vinane **(8)** vya Wilaya za Njombe, Wanging'ombe, Mufindi, Bagamoyo na Muheza. Pia, mradi wa EAAPP umeendeleza utafiti wa kuboresha uzalishaji wa ng'ombe katika kituo cha TALIRI Mpwapwa kwa njia ya uhimilishaji kwa kutumia jumla ya ng'ombe **125.** Vilevile, jumla ya sampuli **54** za vyakula vya mifugo, **52** za maji na **44** za maziwa zilipimwa ili kubaini ubora na usalama wake. Aidha, Wizara ilipitia andiko na mpango wa shughuli za utafiti wa mradi wa EAAPP na kutoa mafunzo kwa wadau **74** kuhusu ubora na usalama wa vyakula na maziwa.

109. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/2016, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo

kuimarisha utoaji huduma za ugani kwa wafugaji na wavuvi:-

(i) Kuandaa na kurusha hewani vipindi **52** vya radio na **12** vya luninga juu ya ufugaji bora wa mifugo, ukuzaji viumbe kwenye maji na uvuvi endelevu;
(ii) Kuendelea kutoa elimu kwa wafugaji na wavuvi **10,000** na kukamilisha ukarabati wa kituo cha Maarifa ya Mifugo cha Lugoba (Bagamoyo); na
(iii) Kutoa huduma za ugani na mafunzo ya ufugaji wa samaki na uvuvi endelevu kwa wadau **250** katika Halmashauri tano (**5**).

### 4.8 Usimamizi wa Ubora wa Mazao na Huduma za Mifugo na Uvuvi

**Bodi ya Nyama Tanzania**

110. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, wizara imeendelea kuimarisha Bodi ya Nyama Tanzania kwa kuipatia wataalam saba (**7**) na vitendea kazi. Aidha, Bodi imeendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu Sheria ya Nyama Sura 421 kupitia vipindi vya redio saba (**7**), kimoja (**1)** cha luninga na vipeperushi nakala **4,500**. Pia, Bodi imefanya tathmini ya uzalishaji na mahitaji ya nyama katika Mamlaka

za Serikali za Mitaa **16** za Ilemela, Nyamagana, Bunda, Bariadi, Serengeti, Kilindi, Korogwe, Jiji la Tanga, Jiji la Arusha, Simanjiro, Kiteto, Temeke, Ilala, Kinondoni, Morogoro na Kilombero. Matokeo yanaonyesha kuwa kuna mahitaji ya tani **163,773** za nyama ikilinganishwa na uzalishaji wa sasa wa tani **106,597** za nyama kwa mwaka ikiwa ni upungufu wa asilimia **35.** Vilevile, Bodi imetambua na kusajili wadau **18** katika Halmashauri za Kwimba, Ilala, Kinondoni, Temeke, Jiji la Arusha, na Chama kimoja (**1**) cha Wafanyabiashara wa Mifugo na Nyama (MWACIBA) katika Jiji la Mwanza.

111. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Bodi ya Nyama imeendelea kufuatilia uingizaji na uuzaji wa nyama na bidhaa zake ambapo jumla ya tani **23.4** za nyama ya ng'ombe, tani **1,388.9** za nyama ya mbuzi na tani **36.7** za nyama ya kondoo zilikaguliwa na kuuzwa katika nchi za Msumbiji, Vietnam, Oman, Qatar na Falme za Kiarabu. Aidha, jumla ya tani **735** za nyama ya ng'ombe, tani **804** za nyama ya nguruwe na tani **16.5** za nyama ya kondoo ziliingizwa nchini. Vilevile, Bodi imeendesha vikao vinne (**4**) vya Bodi na kikao kimoja (**1**) cha Baraza la Mwaka la Wadau wa Tasnia ya Nyama.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuiwezesha Bodi ya Nyama kusajili wadau **5,000** wa tasnia ya nyama na vyama vyao; kuhamasisha utekelezaji wa Sheria ya Nyama Sura 421 na kusimamia ubora wa mifugo, nyama na bidhaa zake na kusimamia biashara na kutafuta masoko ya mifugo, nyama na bidhaa zake ndani na nje ya nchi. Aidha, Bodi itatoa mafunzo kuhusu taratibu za uchinjaji, usafi na utunzaji wa nyama kwa watumishi **39** kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopo katika mikoa **13**. Pia, itawezesha wadau watano (**5)** kushiriki katika maonesho mbalimbali ya mifugo. Vilevile, itaimarisha vyama vya Wafanyabiashara wa Mifugo na Nyama Tanzania (TALIMETA), Wasindikaji wa Nyama Tanzania (TAMEPA) na Wafugaji Tanzania (CCWT) kwa kutoa ushauri, mafunzo na kuratibu maendeleo ya vyama hivyo.

**Bodi ya Maziwa Tanzania**

113. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kuiwezesha Bodi ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kusimamia, kuendeleza na kuratibu tasnia ya maziwa kwa mujibu wa Sheria ya Maziwa Sura ya 262. Aidha, Bodi imeelimisha na kuhamasisha wadau **177** kuhusu Sheria ya Maziwa na kusajili wadau **192.** Pia, Bodi ilitoa

mafunzo ya kuwaandaa wakaguzi ili wapate mbinu za kufanya ukaguzi na kupitia mifumo itakayotumika katika ukaguzi kwa wakaguzi **18** wa maziwa walioteuliwa ambao walipata mafunzo hayo katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Tanga. Vilevile, Bodi iliwatambua watoa huduma **15** kutoka katika Halmashauri za Handeni, Kilosa, Lushoto na Mvomero ambao kwa kushirikiana na Bodi walitoa mafunzo ya kuzingatia usafi na ubora wa maziwa kwa wafanyabiashara wapatao **100** katika mikoa ya Morogoro na Tanga.

114. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi imeendelea kuratibu Programu ya Unywaji wa Maziwa Shuleni katika shule **18** na wanafunzi **14,788** ambao hutumia lita **7,394** za maziwa kwa wiki. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na Manispaa ya Kinondoni imeanza utaratibu wa kuanzisha mpango wa unywaji maziwa kwenye shule kumi **(10)** katika Manispaa ya Kinondoni. Pia, Bodi inaandaa ili kushiriki katika Wiki ya Maziwa itakayofanyika Babati, Manyara ikiwa na kauli mbili ya **'Ng'ombe wa Maziwa ni fursa ya kiuchumi na lishe: Fuga Kisasa'**.

115. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Bodi itaendelea kuelimisha wadau wa maziwa kuhusu Sheria ya Maziwa Sura ya 262 na kusimamia, kuwajengea uwezo wakaguzi **50** wa maziwa kutoka Halmashauri za mikoa ya

Iringa, Njombe na Mbeya na kuhamasisha Halmashauri kutekeleza mpango wa unywaji wa maziwa shuleni na kuratibu maadhimisho ya Wiki ya Maziwa yatakayofanyika kitaifa katika Mkoa wa Njombe.

**Baraza la Veterinari Tanzania**

116. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania imeendelea kusimamia taaluma, viwango na miongozo ya utoaji wa huduma za mifugo kwa kuzingatia Sera na Sheria ya Veterinari Sura 319. Aidha, imeendelea kuimarisha ukaguzi wa huduma za mifugo na kuhamasisha ushirikishwaji wa wataalam wa sekta binafsi katika kutoa huduma. Katika mwaka 2014/2015, Baraza limesajili Madaktari wa Mifugo **38** na kufikisha idadi ya madaktari **719** waliosajiliwa. Pia, Baraza limeandikisha na kuorodhesha wataalam wasaidizi wa mifugo **302**. Vilevile, Baraza limesajili vituo vya kutoa huduma **200**, wakaguzi wa nyama **180,** wahimilishaji **20** na wateknolojia wa maabara **10** wamepatiwa leseni za kutoa huduma kwa wafugaji.

117. ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limekamilisha uandaaji wa Mwongozo wa Kusimamia Mafunzo ya Wataalam wa Afya ya Mifugo na umeanza kutumika. Aidha, ukaguzi wa vituo na huduma za afya ya mifugo umefanyika katika Mamlaka

za Serikali za Mitaa **90** zilizoko katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Kagera, Kilimanjaro, Manyara, Morogoro, Mwanza, Pwani, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga. Pia, ukaguzi na uhamasishaji juu ya viwango vya mitaala ya kufundishia wataalam wa afya ya mifugo umefanyika katika vyuo **11** vinavyotoa mafunzo ya taaluma ya veterinari.

118. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara kupitia Baraza itaendelea kuimarisha ukaguzi wa maadili ya watoa huduma za afya ya mifugo. Aidha, Baraza litasajili madaktari wa mifugo **50**, kuandikisha na kuorodhesha wataalam wasaidizi **1,000**, kutoa leseni kwa watoa huduma na vituo vya afya ya mifugo **400** na kuhakiki mitaala ya mafunzo kwa wataalam na wataalam wasaidiizi wa mifugo ili kuboresha huduma za mifugo zinazotolewa.

**Uthibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi**

119. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia ubora, viwango na usalama wa mazao ya uvuvi pamoja na huduma za kitaalam ikiwemo kufanya uchunguzi wa kimaabara na kaguzi mbalimbali za kuhakiki ubora wa mazao ya uvuvi katika viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi, mialo,

masoko pamoja na vyombo vya kusafirisha mazao ya uvuvi ikiwemo magari na boti. Katika mwaka 2014/2015, Wizara imeanzisha vituo saba (**7**) vipya vya Uthibiti Ubora wa Mazao ya Uvuvi vya Geita, Namanga, Tunduma, Kasanga, Buhingu, Kipili na Ikola na kufanya jumla ya vituo **15**.

**Usimamizi na Ukaguzi wa Viwanda, Maghala, Mialo na Masoko ya Samaki**

120. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara imefanya kaguzi **4,995** kwa lengo la kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi ambapo kaguzi **2,350** zilifanyika wakati wa kusafirisha mazao ya uvuvi kwenda nje ya nchi, kaguzi **462** kwenye viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi, kaguzi **130** kwenye maghala ya kuhifadhi mazao ya uvuvi, kaguzi **1,440** kwenye mialo, kaguzi **13** kwenye masoko na kaguzi **600** kwenye maboti na magari ya kubebea mazao ya uvuvi. Vilevile, jumla ya kaguzi **2,600** zilifanyika kuhakiki ubora na usalama wa samaki zilizoingizwa nchini. Matokeo ya kaguzi hizo yalionesha kukidhi viwango vya ubora vya kitaifa na kimataifa na hivyo viwanda na maghala hayo kuruhusiwa kuendelea na shughuli za uchakataji na uhifadhi wa mazao ya uvuvi. Aidha, Wizara imeendelea kutoa mafunzo kuhusu taratibu na kanuni za usafirishaji wa samaki hai nje ya nchi

na teknolojia sahihi ya uhifadhi na utunzaji wa samaki kwa wasafirishaji wadogo **(25)** na wafanyabiashara (**76**) wanaoingiza mazao ya uvuvi nchini.

121. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu njia bora za uchakataji na uhifadhi wa samaki na mazao yake kwa viwanda **48** vya kuchakata mazao ya uvuvi vilivyopo katika Ukanda wa Bahari ya Hindi (**36),** Ziwa Victoria **(11)** na Ziwa Tanganyika (**1**) ili viweze kuzalisha mazao yanayokidhi vigezo vya kitaifa na kimataifa vya ubora na usalama kwa mlaji.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kutoa elimu na kuhamasisha wadau kuwekeza zaidi katika viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi ili kuongeza uzalishaji na thamani ya mazao ya uvuvi. Pia, kuratibu usimamizi wa usafi kwenye mialo na masoko ya samaki kwa kufanya kaguzi **150** za kina kwenye viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi, kuendelea kutoa elimu na kuhimiza uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi. Aidha, itafanya kaguzi **4,000** za ubora wa samaki na mazao yake kwenye mialo, viwanda na masoko wakati wa kusafirisha nje ya nchi.

**Huduma za Ukaguzi wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi**

123. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha Maabara ya Taifa ya Uthibiti wa Ubora wa Mazao ya Uvuvi – Nyegezi (Mwanza) kwa kuipatia watumishi na vitendea kazi. Pia, Maabara ya uchunguzi wa mwani wenye sumu (*Harmful Algal Blooms)* iliyopo Dar es Salaam imefanyiwa maboresho. Katika mwaka 2014/2015, jumla ya sampuli **998** za samaki, maji, vyakula vya samaki na udongo zilifanyiwa uchunguzi wa kimaabara ili kubaini uwepo wa vimelea vinavyosababisha magonjwa na mabaki ya viuatilifu, madini tembo na madawa ya tiba (kwa samaki wa kufugwa) katika Maabara ya Taifa ya Uvuvi Nyegezi - Mwanza na zile za nje. Matokeo ya chunguzi hizo yameonesha kukidhi viwango vya ubora na usalama kwa afya ya mlaji.

124. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara iliimarisha Maabara ya Taifa ya Uvuvi Nyegezi (Mwanza) na Maabara ya Kuchunguza Mwani wenye Sumu ya Dar es Salaam ambapo watumishi **18** wamepatiwa mafunzo ya kutumia mashine za kupima na kuthibitisha uwepo wa viuatilifu kwenye samaki na maji (**4**), uchunguzi wa viuatilifu (**4**) na mbinu za kuchukua sampuli (**8**). Pia, watendaji wawili (**2**) walipata mafunzo ya menejimenti ya

maabara. Aidha, watumishi **47** wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi kuhusu Kudhibiti Ubora na Viwango vya Mazao ya Uvuvi (**15**) na **32** wamepata mafunzo kuhusu Viwango vya Kimataifa vya ukaguzi wa ndani wa mfumo wa usimamizi wa uzalishaji na uchakataji wa mazao ya uvuvi kulingana na viwango vya kimataifa (**ISO/IEC 17020**). Vilevile, watumishi **4** wanaendelea na mafunzo ya Shahada ya Uzamivu (**1**) na Shahada ya Uzamili (**3**) katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.

125. ***Mheshimiwa Spika,*** katika 2014/2015 Wizara imeiwezesha Maabara ya Taifa ya Uvuvi Nyegezi upande wa Kemikali kukamilisha hatua za kupata Ithibati (*Accreditation*) kwa ajili ya kuhakiki viwango vya mabaki ya kemikali za sumu (*pesticide residues*) na madini tembo (*heavy metals*) kwenye chakula, maji na matope. Aidha, maabara imeendelea kujipima kiutendaji kwa kufanya *Proficiency Testing* kwenye uchunguzi wa madini tembo na matokeo yake yanaonesha kuwa ina uwezo wa kutoa majibu yanayokubalika kimataifa. Pia, kupitia Mradi wa Mazingira wa Ziwa Victoria (LVEMP II) na Programu ya Kuboresha Biashara ya Mazao ya Kilimo (TASP II) inayofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya, vifaa vya maabara vimenunuliwa na majengo yanaendelea kujengwa na kazi hii imekamilika kwa asilimia 80. Vilevile, Miongozo ya kiutendaji imeandaliwa na itawasilishwa

kwenye Taasisi ya kutoa Ithibati kwa ajili ya kuthibitishwa na hatimaye kupewa Ithibati kwa ajili ya uchunguzi wa madini tembo aina nne (Copper, Cadmium, Lead na Chromium).

126. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuimarisha vituo **17** vya Ubora na Uthibiti wa Mazao ya Uvuvi na Maabara ya Uvuvi – Nyegezi kwa kuipatia vitendea kazi na mafunzo kwa watalaam. Aidha, Maabara zitafanya chunguzi za kimaabara kwa sampuli **800** za minofu ya samaki, maji, majitaka na udongo ili kulinda afya ya mlaji. Vilevile, Wizara itaendelea na juhudi za kupata Ithibati kwa upande wa Maabara ya Kemikali.

### 4.9 Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi

127. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuimarisha usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi nchini, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Maji, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Katiba na Sheria, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Halmashauri na Jamii za Wavuvi (BMUs) katika kudhibiti vitendo vya uvuvi haramu,

uharibifu wa mazingira na utoroshaji wa samaki na mazao yake maeneo ya mipakani.

## Udhibiti wa Uvuvi Haramu

128. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kuimarisha vituo **23** vya doria na kuanzisha vituo viwili (Buhingu na Namanga) na hivyo kufanya jumla ya vituo **25** nchi nzima. Vituo hivyo ni pamoja na Namanga, Singida, Mtwara, Dar es Salaam, Mwanza, Bukoba, Mafia, Kilwa, Musoma,Tanga, Kigoma, Mbamba Bay, Murusagamba, Buhingu, Ikola, Horohoro, Kipili, Kasanga, Sota, Sirari, Kasumulo, Tunduma, Rusumo, Kabanga na Kanyigo. Vituo hivyo vimeimarishwa kwa kupatiwa watumishi pamoja na vitendea kazi zikiwemo jenerata tatu **(3)**, gari moja **(1),** pikipiki tatu **(3)** na mafunzo kwa watumishi. Vilevile, ukarabati wa majengo umefanyika kwa vituo vya Bukoba, Dar es Salaam, Mtwara, Mbamba Bay, Musoma Mwanza na Tanga.

Aidha, jumla ya doria zenye siku kazi **5,985** zilifanyika katika Ukanda wa Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Bahari ya Hindi ambazo ziliwezesha kukamatwa kwa zana haramu zikiwemo nyavu za kokoro **544**, kamba za kokoro zenye urefu wa mita **236,750**, nyavu za makila zenye macho madogo **7,921**, nyavu za dagaa **230**, nyavu za utali **12,222**, vyandarua

vya mbu **91**, nyavu za kimia **7**, katuli **19**, nyavu za mtando **12**, mabomu **74**, Mitungi ya gesi ya kuzamia **5**, jozi **42** za viatu vya kuzamia, mitumbwi **359**, injini za mitumbwi **10**, madeli (*cool boxes*) **3**, magari **5** na pikipiki **3**.

129. ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya kilo **34,232** za samaki wachanga, kilo **94** za samaki waliovuliwa kwa mabomu, kilo **140** za majongoo bahari, kilo **62** za mabondo, kilo **35** za kaa na kilo **25** za dodoji (*seahorse)* zilikamatwa. Pia, jumla ya watuhumiwa **447** walikamatwa kutokana na makosa mbalimbali ya uvunjaji wa Sheria na Kanuni za Uvuvi ambapo kesi **16** zimefunguliwa katika mahakama mbalimbali nchini. Aidha, Wizara kupitia Programu ya SmartFish imejenga uelewa kuhusu mfumo wa ulipaji wa leseni za uvuvi kwa njia ya simu kwa Maafisa Uvuvi wa Halmashauri za Wilaya **16** kutoka Ukanda wa Pwani, Maafisa Uvuvi wanane (**8**) kutoka Makao Makuu ya Wizara pamoja na Wakurugenzi Watendaji katika Halmashauri husika. Vilevile, mafunzo ya doria kwa vitendo yalifanyika kwa Maafisa Uvuvi kutoka Halmashauri za mwambao wa Bahari ya Hindi katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Lindi, Pwani pamoja na vikosi vya Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi ambapo jumla ya washiriki **140** walihusika. Mafunzo hayo yaliwezesha kukamatwa kwa vyombo **468**, wavuvi **1,065,** makokoro **9**, nyavu za makila **1**,

nyavu za macho madogo **550**, mbolea ya chumvichumvi kilo **15** , zana za milipuko vipande (*detonator*s) **10**, majongoo bahari kilo **60**, mitando **2,** na mita **20,000** za kamba za kuvutia kokoro. Pia, mafunzo mbalimbali kuhusu Sera, Usimamizi wa Sheria na Kanuni za Uvuvi, Uvuvi endelevu na madhara yatokanayo na uvuvi haramu yalitolewa kwa wadau wa uvuvi **276** katika Kanda za Ziwa Tanganyika (**176)** na Pwani ya Bahari ya Hindi (**100).**

130. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kuratibu na kusimamia uvunaji endelevu wa rasilimali za uvuvi na kudhibiti biashara haramu ya mazao ya uvuvi kwa kufanya doria zenye siku kazi **6,000.**

131. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri pamoja na taasisi mbalimbali na mashirika yasiyo ya kiserikali ikiwemo WWF na Shirika la *Nature Conservancy* la mkoani Kigoma imewezesha kuanzisha Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (*Beach Management Units - BMUs*) **7,** Mto Kilombero **(4)** na Wilaya ya Uvinza (**3**) na kufanya idadi ya BMUs nchini kufikia **749.** Aidha, wavuvi **641** kutoka Halmashauri za Wilaya za Pangani, Tanga mjini, Mtwara Mikindani, Mtwara, Bagamoyo na Mkinga

wamepatiwa mafunzo kuhusu athari za Uvuvi haramu na usimamizi wa rasilimali za Uvuvi unaozingatia ikolojia na mazingira.

132. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo viongozi wa BMUs na Serikali za vijiji kwa BMUs **12** katika wilaya za Mtwara (**2**), Temeke (**5**) na Uvinza (**5**). Aidha, BMUs mbili **(2)** ziliwezeshwa kuandaa Mpango wa usimamizi wa raslimali za Uvuvi katika Halmashauri ya Mtwara. Vilevile, BMUs nane (**8)** za Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji zilihamasishwa na kupewa jukumu la kukusanya ushuru utokanao na mazao ya uvuvi kwa niaba ya Halmashauri.

Katika mwaka 2015/2016 Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri pamoja na wadau mbalimbali itawezesha uanzishwaji wa vikundi **10** (BMUs) na kuimarisha vilivyopo ili kuhakikisha usimamizi imara wa rasilimali za uvuvi unaozingatia matumizi endelevu na ikolojia.

## Usimamizi wa Uvuvi katika Bahari Kuu

133. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara inayosimamia masuala ya uvuvi katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, imefanya doria za anga katika Bahari Kuu ya

Tanzania kwa saa **144** (*manhours*) ili kudhibiti uvuvi haramu. Vilevile, Mamlaka imeshiriki katika doria za kikanda za majini chini ya uratibu wa Sekretariati ya nchi wanachama wa Kamisheni ya Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Commission*). Doria hizo zimeshirikisha nchi za Kenya, Ufaransa, Reunion, Madagascar, Mauritius na Tanzania. Jumla ya saa **8,640** zimetumika katika doria hizo. Pia, ukaguzi wa meli **11** za uvuvi aina ya *purse seiner* na *long liner* ulifanyika katika Bandari za Zanzibar, Mombasa, Mahe Victoria (Ushelisheli) na Mauritius. Katika ukaguzi huo meli zote zilikidhi masharti ya leseni za uvuvi wa Bahari Kuu ya Tanzania. Aidha, leseni **88** za uvuvi wa Bahari Kuu zilitolewa na kuingiza **Dola za Kimarekani 1,863,470** sawa na takribani Shilingi **bilioni 3.3** ikiwa ni ada za leseni za meli za uvuvi kutoka mataifa ya China, Jamhuri ya Korea, Hispania, Mayotte, Taiwan, Thailand, Tanzania, Japan, Oman, Ufaransa na Ushelisheli.

134. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka kwa kushirikiana na Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi, Kampasi ya Mbegani *(Fisheries Education and Training Agency- FETA)* imeendelea kutoa mafunzo kwa wavuvi (**100**) kwa mchanganuo wa wavuvi **50** kutoka Tanzania Bara na **50** kutoka Zanzibar kuhusu nadharia na vitendo vya uvuvi aina ya *long liner na purse seiner*, usalama baharini na uokoaji wa

maisha baharini, uvuvi endelevu, zana rafiki za uvuvi, kulinda rasilimali za uvuvi na mazalia ya samaki na kukusanya takwimu za uvuvi.

Vilevile, Mamlaka imeingia kwenye makubaliano na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) kufanya utafiti wa kutambua maeneo muhimu ya uvuvi ili kuwasaidia wavuvi kutambua maeneo yenye rasilimali nyingi katika Bahari ya Hindi kwa lengo la kuwapunguzia gharama za kutafuta samaki baharini. Pia, Mamlaka imeingia kwenye makubaliano na TAFIRI ya kufanya tathimini ya vifaa vya kuvutia samaki kwenye maji (*Fish Aggregating Devices - FADs)* vilivyowekwa kwenye maji ya kitaifa.

Katika mwaka 2015/2016, Mamlaka itashiriki katika kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni za Uvuvi wa Bahari Kuu na kuboresha mfumo wa kufuatilia meli zinazovua katika Bahari Kuu (*Vessel Monitoring Sytem - VMS).* Vilevile, kwa kushirikiana na Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi Kampasi ya Mbegani itatoa mafunzo ya Uvuvi wa Bahari Kuu kwa wavuvi **50**, kuendesha doria za anga na itahamasisha wadau kuwekeza kwenye Uvuvi wa Bahari Kuu. Aidha, Mamlaka itaendelea kushirikiana na nchi wanachama wa Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi wa Samaki aina ya Jodari katika Bahari ya Hindi ya (*Indian Ocean Tuna Commission)*, Mashirika ya Kikanda na Kimataifa katika

usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za Uvuvi wa Bahari Kuu na usimamizi wa mazingira.

**Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu**

135. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/15 Wizara imeendelea kusimamia na kuhifadhi rasilimali za uvuvi kupitia kitengo chake cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU). Doria zenye jumla ya siku kazi **362** zilifanyika katika eneo la kilometa za mraba **2,000** kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu kwenye Hifadhi za Bahari (**3**) na Maeneo Tengefu (**15**), ambapo mitumbwi **11**, nyavu za timba (kioo) **35**, magunia ya mkaa tisa (**9**), nyavu za tandilo (3), ndoano (**14**), zurumati mbili (**2**), mikuki **20**, nyama ya kasa kilo **10**, baruti kilo **50**, detonator mbili (**2**), fuse mbili (**2**), na chupa (**1**) ya plastic yenye mbolea ya urea vilikamatwa. Vilevile, miti ya mikoko **280**, mbao (**25**) na magogo ya mikoko **15** vilikamatwa na vilitaifishwa kwa amri ya Mahakama. Pia, watuhumiwa watano (**5)** walifikishwa mahakamani na kesi zao ziko katika hatua mbalimbali za kusikilizwa.

Aidha, Kitengo kiliendelea kutangaza vivutio vya utalii vilivyomo katika maeneo yaliyohifadhiwa kwa wawekezaji na wadau wengine kwa kushiriki katika maonesho ya Sabasaba,

Sikukuu ya Wakulima Nanenane, Karibu na Siku ya Mvuvi Duniani. Vilevile, Kitengo kimesaini mikataba minne (**4**) ya uwekezaji wa *"eco-lodge"* katika Maeneo Tengefu ya Shungimbili – Mafia, Kirui/Mwewe – Tanga na Mbudya – Dar es Salaam.

136. ***Mheshimiwa Spika***, Kitengo kiliendelea kufuatilia raslimali za bahari ili kubaini viwango vilivyofikiwa katika uhifadhi wa raslimali na kuratibu shughuli za tafiti katika Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu, ambapo jumla ya viota **10** vya kasa vilitambuliwa na kati ya hivyo viota vitano (**5**) vilivyokuwa na mayai **295** vilianguliwa na kutoa watoto wa kasa **209** na mayai **86** yaliharibika.

Aidha, ufuatiliaji na ukusanyaji wa takwimu za nyangumi ulifanyika katika maeneo ya Hifadhi. Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Novemba, 2014 jumla ya safari za ufuatiliaji **77** zilifanyika ambapo, nyangumi **464** walionekana kati yao **214** ni nyangumi wakubwa na **150** walikuwa watoto. Vilevile, mafunzo yalitolewa kwa wakusanya takwimu za nyangumi **11** ili kuongeza ufanisi wao katika uchukuaji wa takwimu.

137. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kukiimarisha Kitengo kwa kuwawezesha watumishi kuhudhuria mafunzo na kukipatia

vitendea kazi. Katika mwaka 2014/15 watumishi (**11**) wamewezeshwa kuendelea na mafunzo ya muda mrefu kwenye shahada ya uzamivu (**1**), ya uzamili (**5**), ya kwanza (**4**), na stashahada (**1**). Vilevile, Kitengo kimeimarishwa kwa kununua boti (2), injini mbili (2) na kompyuta tatu (3). Aidha, miundombinu ya utalii imejengwa katika Kisiwa cha Toteni – Tanga na Mbudya – Dar es Salaam.

138. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/16 Kitengo kitafanya doria zenye siku-kazi 400 zinazolenga kudhibiti matumizi haramu ya rasilimali za bahari, hususan uvuvi haramu katika Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu. Vilevile, Kitengo kitaendelea kufanya shughuli za uperembaji katika maeneo yaliyohifadhiwa ikiwa ni pamoja na ushirikishwaji wa jamii katika usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi.

Pia, Kitengo kitaendelea kutekeleza Mpango Mkakati (Strategic Plan) wa miaka mitano (2014 -2019) kwa kufanya utafiti na kubaini maeneo yenye sifa za kuhifadhiwa na kuanzisha mchakato wa kuyahifadhi, kutangaza vivutio vya utalii vilivyomo katika maeneo ya uhifadhi kwa wawekezaji na wadau wengine, kutoa mafunzo kwa jamii zinazozunguka maeneo yaliyohifadhiwa na kusaidia katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ili

kuwezesha matumizi endelevu na kupunguza utegemezi uliokithiri wa rasilimali za bahari.

**Uwekezaji kwenye Sekta ya Uvuvi**

139. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uvuvi ikiwemo kuanzisha viwanda vya kuchakata samaki ambapo hadi sasa vimeanzishwa viwanda **48** na maghala **84** ya kuhifadhi mazao ya uvuvi. Aidha, Wizara imeboresha soko la Kasanga (Sumbawanga) na mialo **31** ya kupokelea na kuhifadhi mazao ya uvuvi katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi. Vilevile, Wizara imeimarisha Maabara ya Taifa ya Uvuvi iliyopo Nyegezi (Mwanza) na ile ya Dar es Salaam kwa kuzipatia vifaa vya maabara na kujenga uwezo kwa watumishi.

Pia, Wizara imeendelea kutoa mafunzo kuhusu teknolojia mbalimbali za uhifadhi na uchakataji wa mazao ya uvuvi. Wadau **1,493** kutoka Mikoa ya Mwanza (**185**), Kagera **(180)**, Mara **(150)** na Tanga (**250**), Pwani (180), Dar es Salaam (44), Kigoma (**24**), Mtwara (**52**), Lindi (**78**), Rukwa (**180**) na Katavi (**80**) walinufaika.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** Ili kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi, Wizara inaendelea kuweka mazingira mazuri na

kuboresha miundombinu ya uvuvi. Aidha, Wizara inaendelea na utaratibu wa kumpata Mshauri Elekezi wa kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi ambapo hadidu za rejea zimeandaliwa.

### 4.10 Masuala ya Mtambuka

**Uendelezaji Rasilimali Watu**

141. ***Mheshimiwa spika,*** Wizara imeendelea kusimamia, kuwezesha na kuimarisha rasilimali watu ili itumike kutekeleza na kufikia malengo yake. Katika mwaka 2014/2015 Wizara imeajiri watumishi **182** wakiwemo **68** wa kada za mifugo, **50** kada za uvuvi na **64** kada mtambuka. Aidha, watumishi **311** wamepandishwa vyeo; **13** wamebadilishwa kazi baada ya kupata sifa za Miundo ya Utumishi na **130** wamethibitishwa kazini; **33** wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu kati ya hao, saba (**7**) Shahada ya Uzamivu, **20** Shahada ya Uzamili, sita (**6**) Shahada ya Kwanza na **181** wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi.

142. ***Mheshimiwa spika,*** Wizara imekamilisha mapitio ya Miundo ya Utumishi ya Kada za Mifugo na Uvuvi ili kukidhi mahitaji ya Sekta; kutoa mafunzo kwa watumishi **385** kuhusu kutumia Mfumo wa Upimaji wa Utendaji Kazi wa Uwazi (OPRAS); kutekeleza Mkataba wa

Huduma kwa Mteja; kufanya kikao kimoja cha Baraza la Wafanyakazi na kuelimisha watumishi juu ya maadili na uadilifu. Aidha, watumishi **61** waliwezeshwa kushiriki michezo ya SHIMIWI.

143. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2015/2016 Wizara itaajiri watumishi **298** kati ya hao **147** wa kada za mifugo, **57** kada za uvuvi na **94** kada mtambuka ili kuboresha utendaji wa sekta za mifugo na Uvuvi; **304** watapandishwa vyeo; **137** watathibitishwa kazini na **230** watahudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Pia, watumishi wataendelea kupatiwa vitendea kazi; kupewa elimu juu ya kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za kazi na uadilifu. Aidha, watumishi **65** watashiriki katika michezo ya SHIMIWI na bonanza, kuendesha zoezi la kuhakiki watumishi, kutoa mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya, kusimamia matumizi ya Mfumo wa Upimaji wa Utendaji Kazi wa Uwazi (OPRAS), kufanya vikao **2** vya Baraza la Wafanyakazi na kuwezesha majukumu ya Chama cha Wafanyakazi (TUGHE na RAAWU).

**Utawala Bora, Jinsia na Ukimwi**

144. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kusimamia masuala ya utawala bora, jinsia na UKIMWI kwa kutoa huduma kwa watumishi wenye VVU na

wanaougua UKIMWI na kuhamasisha watumishi **363** kupima afya zao kwa hiari. Aidha, elimu ilitolewa kwa Waelimisha Rika **25**. Kazi nyingine zilizotelelezwa ni:

(i) Kutoa mafunzo kwa watumishi **45** kuhusu namna ya kuferejisha masuala ya jinsia katika mipango ya Wizara;

(ii) Kuratibu na kuwaelimisha watumishi **200** juu ya uadilifu, maadili, wajibu na haki zao;

(iii) Kuelimisha watumishi **870** kuhusu kutekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa;

(iv) Kuchapisha na kutekeleza Mkataba wa Huduma kwa Mteja; na

(v) Kuendelea kusimamia dawati la malalamiko na kufanyia kazi malalamiko yanayotolewa ambapo jumla ya malalamiko **12** yalipokelewa na kupatiwa ufumbuzi.

145. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa na kuhimiza watumishi kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za kazi. Aidha,

Wizara itaendelea kutekeleza Mkataba wa Huduma kwa Mteja na kuimarisha Dawati la Jinsia na Malalamiko. Vilevile watumishi **400** wataelimishwa kuhusu kupima afya zao kwa hiari na kutoa huduma kwa watumishi sita (**6**) wanaoishi na VVU na wanaougua UKIMWI.

**Mawasiliano na Elimu kwa Umma**

146. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 Wizara ilitayarisha na kusambaza taarifa za matukio mbalimbali kuhusu sekta za mifugo na uvuvi kupitia vyombo vya habari. Jumla ya vipindi **9** vya luninga na redio **20** viliandaliwa na kurushwa hewani kuhusu sera, mikakati na mipango ya kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi. Pia, Wizara imesambaza nakala **4,000** za kalenda na **300** za Diaries. Aidha, maktaba ya Wizara imeimarishwa kwa kuipatia watumishi wawili (**2**) na vitendea kazi. Pia, kutoa mafunzo ya dawati la malalamiko kwa watumishi **60** na wadau **31.** Vilevile, mikutano saba (**7**) ya Wizara na waandishi wa habari na wadau ilifanyika kwa lengo la kutangaza majukumu na mafanikio ya Wizara.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuimarisha maktaba ya Wizara; kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara; kuandaa na kurusha hewani vipindi **20** vya luninga na **24** vya redio kutangaza mafanikio ya sekta ya

mifugo na uvuvi; na kuandaa na kusambaza nakala **5,000** za kalenda ya mwaka 2016 na **2,000** za vipeperushi juu ya utekelezaji wa majukumu ya wizara.

**Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**

147. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara imeandaa Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya TEHAMA ya Wizara pamoja na kuimarisha mfumo wa TEHAMA. Pia, Wizara imeunganishwa na Mkongo wa Taifa na kuboresha mawasiliano ya mdahalisi (internet) na kuunganishwa na vituo vya nje kwa lengo la kuweka msingi wa kutumia simu za mdahalisi. Vilevile, Kitengo cha TEHAMA kimewezeshwa kwa kupatiwa watumishi na vitendea kazi.

148. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kujenga mfumo wa kielektroniki wa kukusanya maduhuli ya sekta za mifugo na uvuvi. Aidha, itachapisha Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya TEHAMA. Pia, itajenga mtandao (LAN na WAN) utakaounganisha mawasiliano kati ya Vituo vya Wizara na Makao Makuu. Vilevile, itaendelea kuboresha tovuti ya Wizara kwa lengo la kuwawezesha wadau kupata taarifa mbalimbali za sekta za mifugo na uvuvi na kuwezesha

mafunzo ya stadi za TEHAMA kwa wataalamu wa kitengo.

## Hifadhi ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

149. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) imeendelea kutoa taarifa kwa wafugaji na wavuvi kuhusu upatikanaji wa maji na malisho; hali ya bahari na maziwa na kutoa maelekezo stahiki. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Mradi wa Taifa wa Biogesi, imebainisha maeneo yatakayojengwa mitambo ya mfano ya biogesi inayozingatia hali ya ukame katika mazingira ya ufugaji wa asili katika Wilaya za Arusha, Babati, Longido, Monduli, Hanang, Mbulu, Korogwe, Handeni, Dodoma, Kongwa, Bahi, Kondoa, Singida, Manyoni, Mwanga, Same na Arumeru. Vilevile, Wizara imeendelea kuhamasisha wavuvi juu ya matumizi ya teknolojia zinazozingatia hifadhi ya mazingira na matumizi ya nishati mbadala. Aidha, wadau **132** kutoka kwenye vikundi vya wavuvi wa Wilaya za Muheza, Bagamoyo, Mkinga na Rufiji wamehamasishwa kutumia teknolojia ya kukausha samaki kwa nishati ya jua. Pia, Wizara imeendelea kuhimiza sekta binafsi kuwekeza katika matumizi ya boti za *fibre glass* ili kupunguza ukataji wa miti kwa ajili ya kutengeneza boti za uvuvi.

Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kutoa tahadhari kuhusu mabadiliko ya tabianchi kwa wafugaji na wavuvi na kuhamasisha matumizi ya teknolojia zinazozingatia hifadhi ya mazingira na matumizi ya nishati mbadala. Aidha, itaendelea kuhimiza matumizi ya boti za "*Fibre glass*" ili kupunguza ukataji wa miti kwa ajili ya kutengeneza boti za Uvuvi.

## 5.0 SHUKRANI

150. ***Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara yangu kufanikisha majukumu yake. Napenda kuzitambua na kuzishukuru nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Umoja wa Nchi za Ulaya (EU), Serikali za Australia, Austria, Brazil, Canada, Jamhuri ya Czech, Hispania, Iceland, Ireland, Japan, Jamhuri ya Watu wa China, Israel, Korea Kusini, Marekani, Misri, Norway, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi pamoja na mashirika ya Umoja wa Mataifa ya FAO, IAEA, UNICEF, UNDP, UNIDO na WHO na mifuko ya kimataifa ya GEF na IFAD kwa kuchangia katika maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi.

151. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, nazishukuru taasisi za kimataifa ambazo ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika; Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Japan (JICA), Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Korea (KOICA), Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Shirika la Misaada la Australia (AUSAID), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DfID), Taasisi ya Rasilimali za Wanyama ya Umoja wa Afrika (AU/IBAR), Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE), Shirika la Maendeleo la Uswisi (SDC), Shirika la Ushirikiano la Ujerumani (GTZ), United Nations University (UNU), Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA) kwa michango yao katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi. Pia, nayashukuru Mashirika na Taasisi za hiari za Bill and Melinda Gates Foundation, Association for Agricultural Research in East and Central Africa (ASARECA), The New Partnership for African's Development (NEPAD), International Livestock Research Institute (ILRI), World Wide Fund for Nature (WWF), Indian Ocean Commission (IOC), South West Indian Ocean Fisheries Commission (SWIOFC), Heifer Project Tanzania (HPT), Overseas Fisheries Co-operation Foundation of Japan (OFCF), Vetaid, Care International, OXFAM, Welcome Trust, World Vision, FARM Africa, Land O' Lakes, Building

Resources Across Communities (BRAC), World Society for Protection of Animals (WSPA), Global Alliance for Livestock and Veterinary Medicine (GALVmed), Institute for Security Studies (ISS-Africa), International Land Coalition (ILC), British Gas International, Sea Sense, Indian Ocean Tuna Commission (IOTC), International Whaling Commission (IWC), SmartFish na Marine Stewardship Council (MSC).

152. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa wananchi wote, hususan wafugaji, wavuvi na wadau wengine kwa michango yao katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi nchini. Nachukua nafasi hii kuwaomba waendelee kushirikiana nasi katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi nchini.

153. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nimalizie kuwashukuru kwa dhati Katibu Mkuu **Dkt. Yohana L. Budeba**, Wakuu wa Idara na Vitengo, Taasisi na watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa na kufanikisha maandalizi ya bajeti hii.

## 6.0 BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

154. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2015/2016, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na

Uvuvi ya jumla ya shilingi **68,810,404,000.00** kama ifuatavyo**:-**

(i) Shilingi **46,158,922,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo, shilingi **30,050,702,000.00** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi (PE); na shilingi **16,108,220,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengine (OC); na

(ii) Shilingi **22,651,482,000.00** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, shilingi **22,000,000,000.00** ni fedha za ndani na shilingi **651,482,000.00** ni fedha za nje.

155. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba tena nitoe shukurani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani: *www.mifugouvuvi.go.tz.*

156. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na hotuba hii nimeambatanisha Randama ya Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2015/2016.

157. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI, MHESHIMIWA DKT. TITUS MLENGEYA KAMANI (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016**